# MWONGOZO WA MKUFUNZI WA KUIMARISHA UELEWA WA JAMII KUHUSU RIDHAA INAYOTOLEWA KWA UHURU, KABLA NA BAADA YA KUPATA TAARIFA ZA KUTOSHA

OXFAM
Australia

Kimechapishwa Aprili 2014

Oxfam Australia
132 Leicester Street
Carlton Victoria 3053
Australia
Simu: +61 3 9289 9444
Faksi: +61 3 9347 1983
www.oxfam.org.au

**Mwandishi:** Christina Hill
**Wachangiaji:** Serena Lillywhite na Michael Simon
**Mhariri:** Jane Kunstler
**Msanifu:** Kate Bensen
**Mfafanuzi:** Katie Webber
**Uchapaji:** Eduardo Carbonell

## SHUKURANI:

Oxfam ingependa kuwatambua na kuwashukuru watu wengi ambao wamechangia katika uandaaji wa kitabu hiki cha mwongozo wa mkufunzi wakiwemo wenzetu wa Oxfam: La Chhuon, Kate Geary, Naomi Godden, Emily Greenspan, Gary Lee, Leo van Mulekom, Clair Overy, Jayne Pilkinton, Annie Sloman na Anna Trembath; na Robie Halip kutokana na Makubaliano ya Wenyeji wa Asia; na Helen Tugendhat kutoka katika Programu ya Watu wanaoshughulikia Misitu ambao walipitia mwongozo huu wa mkufunzi.

Shukurani maalumu kwa Hjalmar Joffre-Eichhorn aliyeshirikiana na wafanyakazi na wanafunzi wa chuo kutoka Kituo cha Maendeleo ya Watoto na Mtandao

wa Jamii, na Earth Rights International Mekong School kuanzisha mazoezi ya Jukwaa la Maonyesho yaliyomo katika mwongozo huu. Hjalmar pia ameandika utangulizi kwa miswada iliyomo kwenye Kiambatisho C.

Shukurani zetu za dhati pia ziende kwa Robyn Minty ambaye aliandaa toleo la kwanza la mwongozo huu wa mkufunzi na Wina Kayonga kutoka Kikundi cha Bismarck Ramu; Doreen Tuba, Rowan Naunian na Simon Naikaban kutoka Mfuko wa Maendeleo Vijijini wa Central Sepik; Samson Kubale kutoka PNG Eco Forestry Forum; Augustine Mondu, Gabriel Molok, Jimmy Kalebe, Jimmy Nawik

na Monica Wandarut kutoka Programu ya Maendeleo ya Turubu Eco Forestry; na Lawrence Parime na Lina Wingu kutoka Programu ya Yehimbole Literacy ambaye alitusaidia kukijaribu kiitabu hiki cha mwongozo.

Uandaaji wa kitabu cha mwongozo cha mkufunzi ulisaidiwa na programu ya msaada ya Australia, iliyofadhiliwa na Idara ya Mambo ya Nje na Biashara ya Australia.

Australian Government
Department of Foreign Affairs and Trade

Australian AID

© Oxfam Australia 2014

Oxfam Australia inahusiana na Baraza la Australia la Maendeleo ya Kimataifa (ACFID), ambayo tunafungwa na kanuni zake za maadili; Oxfam International, ambayo tunafungwa na katiba yake na kanuni za maadili; Watu Wanaopata Msaada, ambao tunafungwa na kanuni zao; na Baraza la Wakimbizi la Australia.

Ripoti hii inapatikana kwenye mtandao www.oxfam.org.au/explore/mining/free-prior-and-informed-consent

# YALIYOMO

UKARIBISHO .......... 4
TAARIFA KWA AJILI YA WAKUFUNZI .......... 6
WAJIBU WAKO .......... 6
KUSAIDIA USHIRIKI NA UFANYAJI MAAMUZI WA WANAWAKE .......... 8
1 MIPANGO .......... 10
1.1 KUTATHMINI HATARIZA USALAMA .......... 10
1.2 KUSAIDIA JAMII SAHIHI .......... 11
1.3 KUPANGA PAMOJA NA JAMII .......... 11
1.4 WATU, MAHALI, VITINI NA VIFAA .......... 12
2 UFUNDISHAJI .......... 14
2.1 PROGRAMU YA MAFUNZO INAYOPENDEKEZWA .......... 15
2.2 UJUMBE MUHIMU NA MAZOEZI .......... 16
3 ZANA NYINGINE .......... 40
3.1 VIDOKEZO KWA WAKUFUNZI .......... 40
3.2 KUTATHMINI PROGRAMU YAKO YA MAFUNZO YA FPIC .......... 41
KIAMBATISHO A: MANENO YA JINSIA NA UFAFANUZI .......... 44
KIAMBATISHO B: PICHA ZA MALIASILI KWA AJILI YA ZOEZI LA 4 .......... 45
KIAMBATISHO C: MAONYESHO YA JUKWAANI .......... 51
UTANGULIZI WA MAONYESHO YA JUKWAANI .......... 51
MSWADA WA MCHEZO WA MONYESHO YA JUKWAANI KWA AJILI YA ZOEZI LA 5 .......... 56
MSWADA WA MCHEZO WA MAONYESHO YA JUKWAANI KWA AJILI YA ZOEZI LA 13 .......... 57
KIAMBATISHO D: MATUKIO YA ZOEZI LA 6 .......... 60
KIAMBATISHO E: MASWALI KWA AJILI YA ZOEZI LA 9 .......... 61
KIAMBATISHO F: MIFANO YA UTAFITI WA TATHMINI NA FIKRA BINAFSI .......... 62

# UKARIBISHO

Watu wanapaswa kuwa mstari wa mbele na kiini cha ufanyaji maamuzi ya usimamizi wa maliasili ambayo yanawaathiri. Wanapokabiliwa na uchimbaji madini, ukataji magogo/misitu, mabwawa, mafuta ya mawese, kilimo cha biashara au miradi ya kilimo cha majini, jamii zina haki ambazo lazima ziheshimiwe na serikali zao na makampuni.

Kitabu hiki cha mwongozo wa mkufunzi kiliandaliwa ili kusaidia kuimarisha na kujenga uwezo wa wanaharakati wa jamii, asasi za kiraia (CBOs), asasi nyingine zisizo za serikali (NGOs) na waelimisha jamii ili kuzisaidia jamii kuelewa Ridhaa Inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za Kutosha (FPIC). Inatarajiwa kwamba mwongozo hatimaye utaziwezesha jamii kudai ushiriki muhimu katika kufanya uamuzi wa usimamizi wa maliasili; kwamba michakato ya ndani ya ufanyaji uamuzi wa jamii inajumuisha wanajamii wote; na kwamba miradi itaweza kusonga mbele iwapo tu ridhaa ya jamii iliyoathirika inatolewa.

FPIC inatambuliwa katika Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki ya Wenyeji. Azimio linasema kwamba "Nchi zitaomba ushauri na kushirikiana kwa nia nzuri na wenyeji husika kupitia taasisi zao wenyewe za uwakilishi ili kupata ridhaa yao inayotolewa kwa uhuru, kabla na baada ya kupata taarifa za kutosha kabla ya kuidhinishwa kwa mradi wowote unaoathiri ardhi yao na rasilimali nyingine, hususan kuhusiana na uendelezaji, matumizi au utumiaji wa madini, maji na rasilimali nyingine".[1]

Hata hivyo, FPIC sio suala linalohusu serikali mbalimbali tu. Makampuni pia yanapaswa kuheshimu haki hii. Jukumu la makampuni kuheshimu haki zote za binadamu zinazotambulika kimataifa linaeleweka kwa mapana na kuungwa mkono.

FPIC inataka kwamba watu lazima waarifiwe ipasavyo kuhusu miradi mikubwa kwa muda muafaka na kupewa fursa ya kukubali au kukataa miradi kabla ya kuanza kufanya shughuli hiyo. Hii inajumuisha ushiriki katika kuweka kanuni na masharti ambayo yanashughulikia athari za mradi kiuchumi, kijamii na kimazingira. FPIC inawawezesha watu kujua matokeo ya kufanya maamuzi ambayo yanawaathiri – sio haki tu ya kuombwa ushauri kuhusu miradi ambayo wengine hatimaye watatoa maamuzi yake.

FPIC ni haki mahususi inayoshikiliwa na wenyeji. FPIC inatambua kwamba wenyeji wana haki mahususi za pamoja katika ardhi na inazingatia haki ya uhuru wa kujiamulia mambo yao wenyewe.

FPIC pia inawakilisha maendeleo endelevu ya utendaji bora na kwa hiyo kanuni inayopaswa kulinda utendaji wa serikali na kampuni wakati wanapoomba ushauri na kuzungumza na jamii zote zinazoathirika. Kanuni ambazo zinategemewa na FPIC zinazingatia haki za wote ikiwa ni pamoja na zile za Azimio la haki za Binadamu la Wote, Makubaliano ya Kimataifa kuhusu haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni, na Makubaliano ya Kimataifa ya haki za Kiraia na Kisiasa.

Kwa mfano, watu wote wana haki ya uhuru wa kujieleza, kupata taarifa, na kushiriki katika mwenendo wa masuala ya umma ikiwa ni pamoja na kutumia ushawishi kupitia mjadala wa umma na majadiliano na wawakilishi wao au kupitia uwezo wao wa kujipanga wenyewe. Aidha FPIC inaweza kusaidia kulinda haki zote za watu kwa mali, utamaduni, dini, utafutaji riziki, afya na ustawi wa mwili.

Wakufunzi wanapaswa kutambua kwamba ingawa FPIC inatambuliwa katika sheria ya kimataifa ya haki za binadamu bado ina mjadala mkali na sio wakati wote inatangazwa au kuungwa mkono na wadau wakuu. Kwa mfano:

- Baadhi ya serikali haziungi mkono kwa dhati haki ya wenyeji kwa FPIC ingawa zimeonyesha kuunga mkono Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za wenyej linalodai kwamba FPIC inadhoofisha uhuru wa nchi.
- Baadhi ya serikali hazitambui hadhi ya baadhi ya watu kama wenyeji.
- Baadhi ya serikali haziheshimu haki za raia za kupata taarifa, au kushiriki katika mjadala wa umma.
- Baadhi ya makampuni hayaheshimu haki ya FPIC, hata wakati yanapodai kuheshimu haki za binadamu kwa mapana zaidi, kwa sababu yanaamini kwamba FPIC ni ngumu sana kuitekeleza kwa vitendo na kwamba inaweza kuchelewesha au kuzuia mradi.

[1] Azimio la Umoja wa Mataifa la haki za Wenyeji, ibara 32(2)

Uhalisia ni kwamba mara nyingi jamii zinajikuta zenyewe katika ushindani na serikali yenye nguvu na maslahi ya shirika kwenye ardhi na rasilimali maji. Inaweza kuwa vigumu sana kwa maamuzi ya jamii kuheshimiwa.

— hasa wanapoukataa mradi. Upatikanaji na marekebisho ya kisheria yanayofaa mara nyingi huwa hayapo na mifumo ya udhibiti ambavyo vinapaswa kulinda haki za watu inaweza kuwa dhaifu. Mara nyingi jamii inabidi zitegemee njia zisizo za kisheria ili kulinda haki na maslahi yao, ikiwa ni pamoja na kutoa maamuzi ya maliasili.

Wakufunzi hawahitaji kuwa wataalamu wa sheria kuhusu FPIC ili kutoa mafunzo ya FPIC lakini wanapaswa kuwa na uelewa wa jumla wa mijadala muhimu, hoja za kisheria na sera ya serikali na kampuni na utendaji katika FPIC. Lililo muhimu ni kwamba, wakufunzi wanapaswa kuelewa kwa nini FPIC ni muhimu kwa wenyeji na jinsi inavyoweza kulinda haki na maslahi ya watu wote.

Kitabu hiki cha mwongozo ni andiko kwa ajili ya utendaji wa vitendo wa wakufunzi, kuwasaidia kupanga na kutoa programu za mafunzo ya FPI. Kitabu hiki sio kwa ajili tu ya wakufunzi wenye uzoefu, wawezeshaji au waelimishaji — ni kwa ajili ya watu wanaotaka kuendeleza na kujenga ujuzi na kujiamini kwao katika kuandaa na kutoa programu za mafunzo za FPIC.

Kitabu hiki cha mwongozo kitawasaidia wakufunzi:

- kutoa mafunzo ya ubora wa hali ya juu, yanayofaa ya FPIC;
- kutumia mbinu shirikishi za kujifunza, na zinazozingatia vitendo; na
- kusaidia ushiriki wa dhati wa wanawake katika programu za mafunzo za FPIC, kutambua kwamba wanawake mara nyingi wamekuwa wakiachwa katika michakato ya kufanya uamuzi ya jamii.

Kitabu cha mwongozo cha mkufunzi kinakamilisha Mwongozo wa Oxfam wa Ridhaa Inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya KupataTaarifa za Kutosha.[2]

> Mwongozo wa Oxfam wa Ridhaa Inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya KupataTaarifa za Kutosha unatoa utangulizi wa FPIC na kueleza namna FPIC inavyoweza kuzisaidia jamii kuwa na sauti kuhusu miradi ambayo inaweza kuathiri ardhi, utafutaji riziki na mazingira yao. Mwongozo wa Oxfam wa Ridhaa Inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya KupataTaarifa za Kutosha pia una muundo wa mazoezi ya hatua saba ambazo zinalenga kuzisaidia jamii zilizoathiriwa na mradi kudai kwa pamoja haki zao, kwa vidokezo vyenye manufaa na taarifa nyingine. Mwongozo pia una baadhi ya "bendera nyekundu" zinazoeleza kitu gani kinaweza kutoenda ipasavyo na matatizo ambayo jamii inaweza kukumbana nayo.

Oxfam pia imetoa mfululizo wa Kadi za Ridhaa Inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya KupataTaarifa za Kutosha. Hizi zinaweza kutumika katika programu za mafunzo za FPIC. Zinalenga katika muundo wa hatua saba.

Tunawahamasisha wakufunzi kutumia kitabu hiki cha mwongozo wa mkufunzi na Mwongozo wa Oxfam wa Ridhaa Inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya KupataTaarifa za Kutosha kwa pamoja wakati wa kupanga na kutoa programu za mafunzo za FPIC.

Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi kimegawanywa katika sehemu kuu tatu:

- Sehemu ya 1: Kupanga programu za mafunzo ya FPIC
- Sehemu ya 2: Kuwasilisha programu za mafunzo ya FPIC
- Sehemu ya 3: Zana nyingine kwa ajili ya wakufunzi.

Kitabu cha mwongozo kinaanza kwa baadhi ya taarifa za usuli kuhusu wajibu wa mkufunzi na njia za kuongeza ushiriki wa wanawake katika programu za mafunzo ya FPIC. Kitabu ni kirefu lakini kisiwatie hofu.

Programu za mafunzo ya FPIC zijumuishe ushiriki wa wanawake, wanaume, vijana na wazee katika jamii. Kwa kufanya hivyo, wanajamii wataelewa vizuri haki zao na kuhamasika kushirikiana katika kufanya maamuzi kuhusu miradi ambayo inaweza kuathiri ardhi, utafutaji riziki na mazingira yao.

[2] Inapatikana katika www.oxfam.org.au/explore/mining/free-prior-and-informed-consent
(mwongozo na kadi vimetafsiriwa katika lugha nyingine ambazo pia ziko kwenye tovuti ya OxfamA

# TAARIFA KWA AJILI YA WAKUFUNZI

Sehemu hii inatoa historia zaidi ya kuwasaidia wakufunzi kuelewa wajibu wao, na kuhamasisha ushiriki wa dhati wa wanawake katika programu za mafunzo za FPIC.

## WAJIBU WAKO

Kutoa mafunzo, kuwasilisha na kuwezesha ni dhana sawa na vinakamilishana. Hata hivyo, zina madhumuni tofauti na zinahitaji ujuzi tofauti. Programu ya mafunzo ya A FPIC itajumuisha baadhi ya mafunzo, baadhi ya uwasilishaji na baadhi ya uwezeshaji. Ni muhimu kwamba wakufunzi waelewe kila moja inamaanisha nini.

Kuwasilisha kunahusisha uwasilishaji wa taarifa toka upande mmoja, kutoka kwa mwasilishaji kwenda kwa hadhira

— pamoja na fursa chache (au hakuna) za hadhira kujadili au kushiriki. Kuwasilisha taarifa inamaanisha kwamba idadi ya watu katika hadhira inaweza kuwa kubwa sana.

Mafunzo pia yanajumuisha uwasilishaji wa taarifa lakini kwa njia shirikishi. Mkufunzi anahusisha washiriki katika ujifunzaji wao wenyewe — kwa mfano, kwa kuwahamasisha washiriki kushirikishana na kujifunza kutokana na uzoefu na mawazo ya washiriki wengine. Kimsingi mafunzo yanahusisha watu wachache kuliko inavyowezekana kwa uwasilishaji. Idadi kamili ya washiriki kwa ajili ya programu ya mafunzo ni kati ya watu 20 na 40.

Mkufunzi hapaswi:

- kushauri au kuieleza jamii cha kufanya;
- kujihusisha katika michakato ya utoaji maamuzi ya jamii; au
- kuzungumza kwa niaba ya jamii na wadau wengine.

Uwezeshaji ni mchakato ambao unasaidia kutatua tatizo la kikundi au kupanga mipango ya utekelezaji. Mwezeshaji anasimamia mchakato wa kutatua tatizo au kupanga utekelezaji kwa kutoa muundo katika uchanganuzi na ufanyaji maamuzi wa jamii. Mwezeshaji anaongoza mchakato wa kikundi lakini hausiki na maudhui, majibu au suluhisho la tatizo la jamii.

Kitabu hiki ni mwongozo wa mafunzo. Wakati kinajumuisha baadhi ya mazoezi ambayo yanahusisha uwasilishaji na uwezeshaji, kimelenga katika mafunzo kwa lengo la kuongeza uelewa wa jamii wa FPIC. Mwongozo huu umebuniwa kuwasaidia wakufunzi kuwahusisha wanajamii katika ujifunzaji wao wenyewe. Mwongozo unajumuisha mazoezi (tazama Sehemu 2.2) ambayo yanaweza kutumiwa na wakufunzi kuhamasisha kufikiria kwa kina, kufanya mjadala na uchanganuzi.


Mwongozo unajumuisha zoezi la kupanga mpango wa utekelezaji wa jamii (Zoezi la 18) ili kuzihamasisha jamii kuanza kufikiria kuhusu hatua zipi zinaweza kuhitaji kuzichukua kwa pamoja sasa wakati ambapo wanajua zaidi kuhusu FPIC. Jamii zinaweza kutaka kuandaa mipango ya utekelezaji ya kina zaidi na zinaweza kumuomba mkufunzi kusaidia mchakato huo. Wakufunzi wanahitaji kutambua kwamba hili linahitaji stadi za uwezeshaji, na kuzingatia iwapo wana stadi muhimu za kuzisaidia jamii zaidi ya programu ya mafunzo ya FPIC.

Wakufunzi wanahamasishwa kupanga na kuwasilisha programu za mafunzo za FPIC kama sehemu ya timu ndogo ya mafunzo kuliko kufanya wao wenyewe. Kwa kufanya kazi kama timu, wakufunzi wanaweza kusaidia na kujifunza wao kwa wao na kutumia stadi mbalimbali na uzoefu alio nao kila mkufunzi. Mazoezi mengi katika mwongozo huu yatafanikiwa vizuri kama kuna wakufunzi zaidi ya mmoja ili kuwasaidia washiriki kufanyia kazi mazoezi haya. Kama kuna mkufunzi mmoja tu hii inaweza kusababisha uwasilishaji wa taarifa wenye ushiriki mdogo wa jamii.

Kitabu hiki cha mwongozo wa mkufunzi kimeelekezwa katika mafunzo ya watu wazima kuliko watoto. Watu wazima wote wanajifunza kwa kutofautiana. Kwa mfano, baadhi ya watu wazima wanajifunza kwa kutenda, wengine wanajifunza kwa kutazama na kufikiri, baadhi ya watu wazima wanapendelea nadharia, na wengine wanapendelea jinsi watakavyoweka kujifunza katika vitendo. Kwa hiyo, aina tofauti za mazoezi zinapaswa kujumuishwa katika programu ya mafunzo ambayo inahusisha aina hizi tofauti za kujifunza kwa watu wazima.

Hata hivyo, kitabu hiki cha mwongozo kinaweza kutumiwa na walimu na kubadilishwa kama inavyotakiwa ili kuandaa maandalio ya somo kuhusu FPIC na masuala ya kusimamia maliasili kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya msingi, sekondari na elimu ya juu. Pia mwongozo unaweza kutumika kubuni na kutoa mafunzo kwa wakufunzi wengine (Mfundishe Mkufunzi).

Wakufunzi watathmini kila programu ya mafunzo ya FPIC na vipindi vya utambuzi wa jamii ili kuelewa kama wanajamii wameongeza uelewa wao wa FPIC kutokana na kushiriki kwao katika mafunzo. Tathmini pia itawasaidia wakufunzi kuelewa kitu gani kimekwenda vizuri na kipi kinahitaji kubadilishwa kwa ajili ya programu za mafunzo za siku zijazo. Sehemu ya 3.2 inatoa baadhi ya mifano ya zana za tathmini ambazo zinaweza kutumika.



## KUSAIDIA USHIRIKI NA UFANYAJI MAAMUZI WA WANAWAKE

Wanawake wana haki sawa[3] ikiwa ni pamoja na haki halisi ya usawa katika michakato ya kisiasa, haki ya kusikilizwa sauti zao na haki ya kushiriki katika michakato ya kufanya maamuzi ya jamii na miradi. Kama wanaume, wanawake wana haki ya kunufaika na miradi mikubwa na kuwa salama kutokana na madhara yoyote yanayoweza kuletwa na mradi. Hata hivyo, athari za uchimbaji madini na miradi mingine mikubwa hazizingatii usawa wa kijinsia. Mara nyingi wanawake wanapata athari mbaya kuliko wanaume, na mara chache wanapata manufaa wanayoyapata wanaume.[4]

Kwa mfano:

- Sio wakati wote wanawake wanaombwa ushauri wakati makampuni yanapopatana kupata ardhi;
- Uharibifu wa mazingira unadhoofisha uwezo wa wanawake kutoa chakula na maji safi kwa familia zao na unaweza kuongeza mzigo wao wa kazi;
- Fidia na marupurupu zinalipwa kwa wanaume "kwa niaba ya" familia zao, wakiwanyima wanawake manufaa ya kifedha ya mradi na uwezekano wa kuongeza utegemezi wao kiuchumi kwa wanaume;
- Wanawake wanaweza kupoteza hadhi yao ya kimila katika jamii pale miradi inapoleta uchumi wa fedha taslimu;
- Mwanaume mfanyakazi wa muda, nguvu kazi ya mradi vinaweza kuleta ongezeko la pombe, wafanya biashara ya ngono na ukatili katika jamii, ambavyo vinaweza kuathiri usalama wa wanawake; na
- Mara nyingi wafanyakazi wanawake wanakabiliwa na ubaguzi, mazingira duni ya kufanyia kazi na malipo yasiyo sawa kwa kazi inayofanana.

Mara nyingi wanawake wanakabiliwa na vikwazo vingi vya kushiriki katika kufanya maamuzi.[5] Hata hivyo, wakufunzi wanaweza kusaidia ushiriki wa wanawake katika programu za mafunzo ya FPIC na michakato ya ufanyaji maamuzi ya jamii. Kwa kuanza, wakufunzi wasipuuze, kukubali au kuhusika na ubaguzi dhidi ya wanawake au kuondolewa kwao katika programu ya mafunzo ya FPIC ikiwa ni pamoja na wakati hili linapozingatia utamaduni, dini au "mila". Ndani

ya jamii nyingi, wanawake wamekuwa au kidesturi wana majukumu muhimu ya kufanya maamuzi, ingawa majukumu hayo yanaweza kufanya kazi tofauti katika jamii tofauti. Utengaji wa wanawake lazima upingwe lakini katika namna ambazo zinaheshimu wanajamii wote.

Ushiriki wa wanawake katika programu ya mafunzo ya FPIC ni muhimu kwa kuwa unasaidia wanawake kuelewa na kutetea haki zao, na kulinda maslahi ya jamii nzima.

Katika hatua ya mipango, wakufunzi washirikiane na kikundi cha wanawake kuhakikisha kwamba wanawake wanaweza kushiriki katika programu ya mafunzo ya FPIC na, inatarajiwa, katika michakato ya ufanyaji maamuzi wa jamii. Lengo liwe kwamba wanawake wahusishwe kikamilifu katika mafunzo na kuwa na ushawishi halisi wakati wa mafunzo na baada ya hapo, kuliko tu kufanikisha idadi fulani ya ushiriki wa wanawake katika programu ya mafunzo. Hata hivyo, kiasi wanaweza kuchangia katika wanawake kuweza kushiriki kikamilifu na kuwa na ushawishi.

Wakufunzi na vikundi vya wanawake wazingatie:

- Ni vikwazo gani vya utendaji (mfano, umuhimu wa kulea watoto au kufanya kazi za nyumbani au utafutaji riziki) vinaweza kuzuia ushiriki wa wanawake katika mafunzo na kutafuta njia ya kukabiliana na vikwazo hivyo;
- Ni vikwazo gani vya kiutamaduni vinazuia ushiriki wa wanawake na kutafuta njia ya kukabiliana navyo;
- Jinsi programu ya mafunzo inavyoweza kushughulikia mahitaji ya kujifunza kwa wanawake na maslahi yao.

Wakufunzi na vikundi vya wanawake pia wazingatie idadi fulani (yaani, 50% wanawake, 50% wanaume), wanaedesha programu za mafunzo tofauti kwa wanawake na wanaume, au mkakati mwingine utawawezesha wanawake kushiriki kwa dhati na kuwa na ushawishi. Kama michakato tofauti kwa wanawake na wanaume inakubaliwa, wakufunzi wakutanishe makundi tofauti kushirikishana mitazamo na uelewa wao tofauti. Masuala mengine ya kuzingatia yanajumuisha usalama wa wanawake, na desturi za wanawake na wanaume kujumuika pamoja.

[3] Makubaliano ya Utokomezaji wa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya wanawake.

[4] Oxfam Australia: Wanawake, jamii na uchimbaji madini: The gender impacts of mining and the role of gender impact assessment, resources.oxfam.org.au/pages/view.php?ref=460andk=

[5] Utafiti wa mwisho wa wenyeji na haki ya kushiriki kufanya maamuzi, Report of the Expert Mechanism on the Rights of Indigenous Peoples, A/ HRC/EMRIP/2011/2, 26 May 2011, tazama ukurasa 8 na 21.

Sehemu ya 2 ina programu ya mafunzo inayopendekezwa. Mazoezi mengi yana "ujinsia" — hii ina maana yamebuniwa kuelewa hamu na mitazamo tofauti ya wanawake na wanaume. Hii inatambua kwamba

Uchimbaji madini, ukataji magogo na miradi mingine vinawaathiri wanawake na wanaume kwa tofauti (kwa sababu wanawake na wanaume wana wajibu na majukumu tofauti katika familia na jamii), na kwamba wanawake na wanaume mara nyingi wana mahitaji na maslahi tofauti. Wakufunzi wanahamasishwa kurekebisha programu ya mafunzo iliyopendekezwa na shughuli binafsi kama ni lazima ili kuhakikisha kwamba programu inashughulikia mahitaji na maslahi ya wanawake.

Wakati wa programu ya mafunzo ya FPIC, wakufunzi wanaweza kuhamasisha ushiriki kikamilifu wa wanawake kwa:

- Kuanzisha matarajio ya kuheshimiana, ikijumuisha wanaume kuwaheshimu wanawake na kusikiliza watakachokisema;
- Kuhakikisha kwamba wanawake wana nafasi ya kukaa kwenye chumba cha mafunzo (sio nje au mahali wasipoweza kusikia au kuchangia majadiliano);
- Kuwaruhusu wanawake kujibu maswali, kuripoti kutoka kwenye mazoezi ya kikundi, n.k.; na
- kufuatilia mafunzo, kama matatizo yatajitokeza, kuhakikisha kwamba utatuzi unafanyika; kwa mfano, kama wanaume wanahodhi shughuli za kikundi kidogo au majadiliano, zingatia kuunda vikundi tofauti vya wanawake na wanaume kuzungumza baina yao kwa namna salama na ya kusaidia.

Timu za mafunzo zijumuishe wakufunzi wanawake na wanaume. Wakufunzi wanawake wawe wenzi sawa katika mipango na utoaji wa mafunzo — wajibu wao usizuiwe kuandaa lojistiki au kutoa chakula cha mchana siku ya mafunzo.

Wakufunzi wanaweza kutaka kufanya baadhi ya mafunzo ya jinsia wenyewe ili kujenga uelewa wao wenyewe, stadi na kujiamini katika masuala ya jinsia. Wakufunzi wanaweza kuanza mchakato huu kwa kujiuliza wenyewe:

- Kwa nini tunafikiri ushiriki wa wanawake, sauti na ufanyaji maamuzi ni muhimu?
- Wanawake wana mchango gani katika asasi yetu wenyewe? Kwa nini imekuwa hivyo?
- Ndani ya jamii, je, kaida za kiutamaduni ni chanzo cha uwezeshaji, ustawi wa jamii na uwezo wa wanawake na wanaume? Kama ni hivyo, kwa vipi?
- Je, utamaduni unatumika kuhalalisha utengwaji wa wanawake au ubaguzi dhidi ya wanawake? Ambao maslahi yao yanawakilishwa kama hivi ndivyo ilivyo?
- Tunaelewa nini kuhusu maneno ubaguzi wa jinsia, usawa wa jinsia, mabadiliko ya jinsia na uwezeshaji wanawake?[6]

Zaidi ya kusaidia ushiriki wa wanawake, wakufunzi pia wasaidie ushiriki wa vijana, watu wenye ulemavu na wengine ambao wanaweza kutengwa katika michakato ya ufanyaji maamuzi ya jamii.

[6] Kiambatisho A kina ufafanuzi wa maneno haya na mengine baadhi

# 1 MIPANGO

Sehemu hii ya mwongozo inawasaidia wakufunzi kupanga programu zao za mafunzo za FPIC. Mipango ni muhimu kama ilivyo utoaji wa mafunzo yenyewe. Programu ya mafunzo itafanikiwa tu kama muda wa kutosha utawekwa katika hatua ya kuweka mipango.

Sehemu muhimu ya mipango ni kuhakikisha kwamba jamii inaelewa wakufunzi ni akina nani na mafunzo ni kwa ajili ya nini, na kwamba wakufunzi wanaelewa jamii ni ipi na muktadha wa eneo. Jambo la kwanza ambalo wakufunzi wangepeda kufanya ni kuitembelea jamii, zaidi kwa mwaliko wa wanajamii, ili kupata hisia ya inaweza kuwaje kuishi pale — nani anaishi katika jamii, wanafanya nini kwa ajili ya riziki zao, je, kuna mradi wowote unaoanzishwa jirani?

Hatua ya mipango pia ihakikishe kwamba mafunzo yanapatikana kwa wanajamii wote.

— hasa wale wenye uwezekano wa kuathiriwa na mradi na wale ambao kawaida wanatengwa katika michakato ya kufanya maamuzi ya jamii.

Sehemu nyingine muhimu ya mchakato wa mafunzo ni kuhakikisha kwamba programu ya mafunzo inakidhi mahitaji ya washiriki. Sehemu ya 2 ina programu ya mafunzo inayopendekezwa, na ujumbe na mazoezi muhimu. Katika hatua ya mipango, programu hii inaweza kurekebishwa ili iendane na mahitaji ya jamii. Baadhi ya sehemu za programu zitahitaji uzingatiaji mahususi wakati wa hatua ya mipango, kama vile kuandaa kwa ajili ya somo la sheria ya FPIC au kushirikiana na baadhi ya wanajamii kwenye mazoezi ya "Maonyesho ya Jukwaani"

## 1.1 KUTATHMINI HATARIZA USALAMA

Oxfam inatambua changamoto na masuala ya usalama ambayo jamii nyingi na watu binafsi wanakabiliana nayo katika kuhakikisha haki zao zinaungwa mkono na matatizo yanatambuliwa. Wakufunzi pia wanaweza kukabiliwa na changamoto hizo na masuala ya usalama. Wakufunzi wanashauriwa kuzingatia kwa makini hatari za usalama wanapopanga na kufundisha programu za mafunzo za FPIC.

Wakufunzi watambue kwamba wanawake na wanaume wanakabiliwa na hatari tofauti. Kwa mfano, wanawake wanaweza kukabiliwa na kuongezeka kwa hatari, kukihusishwa na sauti kuu na ushiriki katika kufanya maamuzi, kama watashiriki katika mafunzo. Wakufunzi washirikiane kwa karibu na vikundi vya wanawake wenyeji ili kutathmini na kushughulikia hatari hizo.

Wakufunzi wanahitaji kubainisha na kutathmini uwezekano wote wa hatari kwa usalama wao na usalama wa washiriki. Hii inajumuisha hatari zinazohusiana na:

- Kuwepo au uwezekano wa kuwepo kampuni, polisi au watumishi wa jeshi;
- Mgogoro kati ya jamii na kampuni, polisi au jeshi;
- Mgogoro ndani ya jamii na mgogoro baina ya jamii;
- Kusafiri kwenda na kutoka katika jamii; na
- Upatikanaji wa masuala ya hali ya hewa na msimu.

Mara tu hatari inapobainishwa inaweza kupimwa (ni ya chini, ya kati au kubwa?) na mpango wa kushughulikia kila hatari unaandaliwa. Mpango huu wa kutambua na kushughulikia hatari uandaliwe kwa kupata maoni toka kwa jamii.

Kama hatari ni kubwa sana basi hatua inayofaa zaidi kuchukua inaweza kuwa kufuta au kuahirisha programu ya mafunzo. Badala yake, programu ya mafunzo inaweza kufanyika mahali tofauti; kwa mfano, mji wa karibu zaidi kuliko katika jamii, ingawa hii inaweza kuzuia nani anaweza kushiriki katika mafunzo.

## 1.2 KUSAIDIA JAMII SAHIHI

Uamuzi wa kufundisha programu ya mafunzo ya FPIC katika jamii mahususi kwa muda maalumu unafanywa na jamii na wakufunzi. Hata hivyo, wakufunzi wanapaswa kuelewa wazi thamani muhimu ya mafunzo ya FPIC itakayopata jamii kwa wakati huo. Rasilimali chache na vipaumbele vinavyoshindana ni uhalisia.

Kwa mfano, kama hakuna miradi mikubwa lakini waendelezaji wanachunguza eneo hilo au miradi iliyopo inaelekea kupanuliwa, kutakuwa na thamani kubwa kwa jamii za wenyeji kujifunza kuhusu FPIC. Vivyo hivyo, ikiwa msimamizi wa mradi inabidi afanye mchakato wa tathmini ya athari ya mazingira na jamii, kutakuwa na thamani katika mafunzo ya FPIC. Kama ni mradi mkubwa, kama vile mgodi au bwawa, ambao tayari unaendeshwa, jamii bado inaweza

kutaka kujifunza zaidi kuhusu FPIC — na jinsi wanavyoweza kushawishi namna mradi unavyoendeshwa na namna msimamizi wa mradi anavyoweza kujihusisha na jamii siku za baadaye. Kwa upande mwingine, kunaweza kuwa na mzingira fulani ambapo mafunzo ya FPIC yatakuwa na thamani ndogo; kwa mfano, katika mazingira ya mgogoro unaohusiana na mradi.

## 1.3 KUPANGA PAMOJA NA JAMII

Wakufunzi waelewe muktadha, mahitaji na maslahi ya jamii ambapo wanadhamiria kutoa mafunzo ya FPIC. Jamii (au wawakilishi wake) wanapaswa kuelewa wazi wanachoweza kupewa na wakufunzi na nini matarajio ya wakufunzi kwa jamii. Wakufunzi na wawakilishi wa jamii washirikiane kupanga mafunzo. Mipango ihusishe wawakilishi wa wanawake na vijana. Ziara kadhaa katika jamii zinaweza kuwa muhimu katika hatua ya kuweka mipango.

Katika mkutano wa kwanza wakuweka mipango, wakufunzi wanapaswa:

- Kuiambia jamii wao ni akina nani, asasi yao na kwa nini wanapenda kutoa mafunzo hayo;
- Kuieleza jamii ni nani amewaalika kutembelea jamii;
- Kuelezea programu ya mafunzo ya FPIC inahusisha nini na kwamba mafunzo yanalenga kusaidia wanajamii kuongeza uelewa wao wa FPIC;
- Kueleza kwamba programu ya mafunzo ya FPIC haitakuwa na sharti la kutatua matatizo yote ya jamii bali kwamba ni mahali pa kuanzia kwa jamii kuelewa na kutetea haki zao;
- Kuwaeleza wawakilishi wa jamii kwamba ushiriki wa wanawake na wanaume unatarajiwa na kwamba programu ya mafunzo haitaendelea kama wanawake wanazuiwa kushiriki; na
- Kuuliza kama kuna hatari kwa usalama wa wakufunzi na jamii kama mafunzo ya FPIC yatatolewa na, kama ni muhimu, kutafuta maoni katika mpango wa kutambua na kushughulikia hatari.
- Kama itakubalika kwamba mafunzo yataendelea, basi wakufunzi washirikiane na wawakilishi wa jamii, vikiwemo vikundi vya wanawake, katika:
- Kuelewa muktadha mahususi, mahitaji na maslahi ya jamii — pamoja na kama kuna miradi yoyote inayoanzishwa karibu na jamii na ni mtazamo gani au maoni waliyo nayo wanajamii kwa mradi.
- Kuelewa maarifa na ujuzi wa washiriki wa mafunzo wanaotarajiwa, viwango vya kujua kusoma na kuandika na taratibu mahususi za utamaduni wa kujifunza ili mafunzo yarekebishwe kulingana na jamii.
- Kuomba msaada kutoka kwa wawakilishi wa jamii ili kuendeleza mafunzo na kukaribisha watu kuhudhuria, kuhakikisha kuna uwakilishi kutoka kwa wanajamii wote.
- Kueleza kwamba kuna fursa kwa wana jamii kufanya kazi na wakufunzi ili kuandaa na kutoa baadhi ya mazoezi ya programu.
- Kukubaliana na wawakilishi wa jamii kuhusu mahali pa mafunzo, tarehe (ukiepuka muda wenye shughuli nyingi kama vile wakati wa misimu ya kupanda au kuvuna), idadi ya watu wenye uwezekano wa kuhudhuria na masuala mengine ya lojistiki kama vile usafiri, chakula na malazi.

Rasimu ya programu ya mafunzo igawanywe na kujadiliwa na wawakilishi wa jamii na marekebisho hayo yazingatie maoni kutoka kwa wawakilishi wa jamii.

## 1.4 WATU, MAHALI, VITINI NA VIFAA

Unapopanga programu ya mafunzo ya FPIC ni muhimu kuzingatia watu, mahali, vitini na vifaa vya kufundishia ambavyo vinahitajika ili kuhakikisha mafanikio ya programu.

### Watu

Kama ilivyojadiliwa hapo juu, programu bora za mafunzo zinahusisha ushiriki kikamilifu wa wanajamii katika kuamua malengo ya mafunzo, na katika kusaidia kupanga na kufundisha programu. Wanajamii wajue vizuri uwezo wao wenyewe, mahitaji na maslahi, na nini kinatokea ndani ya jamii — utambuzi na uzoefu wao utambuliwe na kujumuishwa kwenye programu.

Kuwajumuisha wanajamii katika mipango ya programu na ufundishaji kutajenga upendeleo wao na umiliki katika mafunzo. Aidha, hii inaweza kuwapa fursa ya kuendeleza baadhi ya stadi na kujiamini (kwa mfano, kuongea mbele ya watu au kusimamia shughuli za kikundi). Wanajamii wanaweza kualikwa kufanya kazi na wakufunzi kuandaa na kufundisha baadhi ya mazoezi ya programu.

Zaidi ya hayo, siku ya mafunzo, wanajamii wanaweza kuombwa:

- Kuandaa mahali pa mafunzo (kwa mfano, kuweka mabango, kupanga viti na meza);
- Kuwakaribisha rasmi washiriki wote na wakufunzi kwenye mafunzo;
- Kugawa vitini vya mafunzo kwa washiriki;
- Kusaidia kuzingatia muda; na
- Kuandaa chakula kwa washiriki — kama wanawake wanahusika na uandaaji wa chakula, huu sio mbadala kwa wanawake wa kushiriki katika programu ya mafunzo.

Kama ilivyopendekezwa awali, fursa za kushiriki kwa wanajamii zielezwe katika mkutano wa mipango na wawakilishi wa jamii. Mkufunzi athibitishe nani anajitolea kwa kazi zipi kabla ya programu ya mafunzo. Wanawake, wanaume na vijana wote wapewe fursa ya kujitolea..

### Mahali pa mafunzo

Programu ya mafunzo ya FPIC ifanyike kwenye jamii kuliko mahali mbali na jamii. Hii itaongeza ushiriki wa wanajamii wote, hasa wale ambao wana majukumu mengine kama vile kulea watoto, kutayarisha chakula cha familia au kulima na shughuli nyingine za kutafuta riziki.

Mahali pa mafunzo patahitaji kuchaguliwa. Mahali pa mafunzo panaweza kuwa bwalo la jumuiya au mahali pa kukutania, shule, jengo la dini au sehemu ya wazi. Mahali pa mafunzo pawe pakubwa pa kutosha kukaa washiriki wote, na kuwa na nafasi ya kufanya mazoezi ya kikundi kidogo na majadiliano. Mambo mengine ya kuzingatia yanajumuisha kama mahali ni tulivu, kama chakula kinaweza kuandaliwa na kama kuna chanzo cha uhakika cha umeme. Mwisho, wanawake wanaweza tu kushiriki katika mafunzo kama uangalizi wa watoto unatolewa, mahali pa mafunzo patahitaji kuweza kulizingatia hilo. Masuala ya usalama pia yanaweza kuhitaji kuzingatiwa.

### Vitini na Vifaa vya mafunzo

Mkufunzi atahitaji vitini na vifaa mbalimbali ili kuhakikisha kwamba programu ya mafunzo ya FPIC inaendeshwa vizuri na kwamba kila mtu anaweza kushiriki kikamilifu. Mkufunzi anaweza kuja na vitu hivyo au vinaweza kuazimwa kutoka kwa mtu katika jamii.

Vitini na vifaa vya mafunzo vinajumuisha:

- kitabu hiki cha mwongozo wa mkufunzi na Mwongozo wa Oxfam wa Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za Kutosha kitakachotumiwa na wakufunzi;
- nakala za Mwongozo wa Oxfam wa Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za Kutosha, kadi za FPIC au zinazofanana kwa kila mshiriki[7];

- nakala za programu ya mafunzo kwa kila mshiriki;
- ubao mweusi au mweupe wa kuandikia na makaratasi makubwa, na kalamu za rangi au chaki;
- rasilimali mahsusi kwa kila zoezi (hii inaweza kuhitaji kurasa zilizolewa fotokopi kutoka kwenye kitabu cha mwongozo kumpa kila mshiriki);
- saa, saa ya mezani au simu ya mkononi kwa ajili ya kuangalia muda;
- kengele, ngoma au kitu chochote kinachoweza kutumika kuvuta usikivu wa washiriki;
- taarifa kuhusu sheria husika za eneo kwa FPIC na usimamizi wa rasilimali, na orodha ya asasi za ndani ambazo zinaweza kutoa msaada endelevu kwa jamii;
- peni, penseli, karatasi isiyoandikwa, karatasi ya rangi, vikaratasi vya kunata, kamba, pini au tepu ya kunata, n.k;
- nakala ya fomu ya tathmini au zana nyingine za kupata maoni ya washiriki;
- mabango, video/DVDs (hiari);
- kompyuta na projekta (hiari); na
- vibandiko vya majina (hiari).

Kama programu ya mafunzo ya FPIC ni ndefu zaidi ya nusu siku, wakufunzi wanaweza kufikiria kutoa chakula kwa washiriki.




[7] Mwongozo wa Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za Kutosha umetafsiriwa katika lugha kadhaa. Hata hivyo, kama hakuna tafsiri kwa lugha inayozungumzwa ambapo mafunzo yanapangwa, wakufunzi wanaweza kutaka kutafsiri mwongozo. Badala yake, wakufunzi wanaweza kutumia lugha ya asili ya maandiko ya FPIC ambayo yameandaliwa na asasi au maandiko yao wenyewe.

# 2 UFUNDISHAJI

Sehemu hii ya kitabu cha mwongozo inawasaidia wakufunzi kufundisha programu zao za mafunzo. Ina ujumbe na mazoezi muhimu. Mazoezi yamebuniwa kuongeza ushiriki wa kikamilifu wa wanajamii katika mafunzo nakuwahusisha washiriki katika kujifunza kwao wenyewe. Imebuniwa kuwa programu ya mafunzo ya siku mbili, Siku ya 1 inajumuisha Zoezi la 1 hadi 9; na Siku ya 2 Zoezi la 10 hadi 19. Mkufunzi anaweza kupenda kujumuisha zoezi fupi la kujipima mwishoni mwa Siku ya 1 ili kuwahamasisha washiriki kufikiria kuhusu namna walivyojifunza siku hiyo na wanachotarajia kupata Siku ya 2.

Hata hivyo, wakufunzi wanaweza kuchagua kuendesha mafunzo kwa siku mbili na nusu au tatu. Hii itaruhusu muda wa ziada kwa ajili ya mazoezi, na mapumziko marefu katika siku hiyo na kuweza kumakinika tena. Hili linaweza kuwa muhimu pale washiriki wanapokuwa na uzoefu mdogo wa mafunzo.

Ni juu ya wakufunzi na jamii kuamua urefu na maudhui ya programu, na kupanga ipasavyo. Programu inaweza kuwa saa chache tu au muda mrefu zaidi kwa siku tatu au nne. Kama programu ndefu inakubaliwa, siku za nyongeza zinaweza kutumika katika kutatua tatizo la jamii na mipango ya utekelezaji kama wakufunzi wako huru kuchukua jukumu hilo.

Wakufunzi wanahamasishwa kutumia ujumbe muhimu na mazoezi kutoka sehemu hii. Hata hivyo, wakufunzi wabadilishe programu, na kurekebisha programu ili kukidhi mahitaji ya jamii na kushughulikia ipasavyo katika muktadha wa eneo. Wakufunzi pia wazingatie viwango vya kutojua kusoma na kuandika na taratibu za jamii za kiutamaduni za kujifunza na kubadilisha mazoezi ipasavyo. Kwa mfano, katika baadhi ya mazoezi inapendekezwa kwamba majadiliano ya kikundi yamewekwa katika maandishi. Hata hivyo, kama viwango vya kujua kusoma na kuandika viko chini, itakuwa vizuri kuandika majadiliano kwa kuchora picha au kulenga katika ripoti ya mdomo kwenye kikundi kikubwa kuliko muhtasari wa kuandika. Masuala haya lazima yashughulikiwe katika hatua ya kuweka mipango.

## 2.1 PROGRAMU YA MAFUNZO INAYOPENDEKEZWA

| Namba na jina la zoezi | | Muda unaopendekezwa kwa zoezi |
|---|---|---|
| Zoezi la 1 | Ukaribisho na utangulizi | Dakika 30 |
| Zoezi la 2 | Makubaliano ya programu ya mafunzo | Dakika 30 |
| Zoezi la 3 | Matarajio ya washiriki | Dakika 30 |
| Zoezi la 4 | Kujipima na majadiliano | Dakika 45 |
| Zoezi la 5 | Ridhaa inayotolewa kwa "Uhuru" | Saa 1 (kiwango cha chini) |
| Zoezi la 6 | Ridhaa inayotolewa "Kabla" | Saa 1 |
| Zoezi la 7 | Ridhaa inayotolewa baada ya kupata "Taarifa za Kutosha" | Saa 1 |
| Zoezi la 8 | FPIC na sheria | Saa 1 |
| Zoezi la 9 | Nini kinatokea kwenye jamii | Dakika 30 |
| Zoezi la 10 | Hatua ya 1 — jua nani anaadaa mradi | Dakika 30 |
| Zoezi la 11 | Hatua ya 2 — omba taarifa kwa msimamizi wa mradi | Dakika 45 |
| Zoezi la 12 | Hatua ya 3 — fanya majadiliano na jamii | Saa 1 (kiwango cha chini) |
| Zoezi la 13 | Hatua ya 4 — mapatano ya jamii na msimamizi wa mradi | Saa 1 (kiwango cha chini) |
| Zoezi la 14 | Hatua ya 5 — tafuta ushauri huru | Dakika 30 |
| Zoezi la 15 | Hatua ya 6 — fanya uamuzi kama jamii | Saa 1 (kiwango cha chini) |
| Zoezi la 16 | Hatua ya 7 — mawasiliano yaliyopo na msimamizi wa mradi | Dakika 30 |
| Zoezi la 17 | Kujifunza kuhusu Hatua 1–7: Uchaguzi B[8] | Saa 2 |
| Zoezi la 18 | Mshiriki kujipima na mipango ya utekelezaji ya jamii | Saa 1 |
| Zoezi la 19 | Tathmini ya programu ya mafunzo na kufunga | Dakika 30 |

Sehemu ya 2.2 ina mazoezi. Kila zoezi linaeleza:

- lengo la zoezi;
- muda unaaopendekezwa ambao zoezi litachukua;
- rasilimali zinazotakiwa kwa zoezi;
- ujumbe muhimu;
- maelekezo kwa zoezi lenyewe; na
- vidokezo zaidi vya kuwasaidia wakufunzi kusimamia zoezi.

Ujumbe muhimu ni taarifa wakufunzi wanayopaswa kuwaambia washiriki. Taarifa itatoa msingi wa zoezi ambalo litafuata na kuhakikisha washiriki wana uelewa wa msingi wa FPIC. Sehemu kubwa ya ujumbe muhimu imechukuliwa kutoka Mwongozo wa Oxfam wa Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya Kupata Taarifa za Kutosha na wakufunzi wanahimizwa kurerejelea humo. Ni kiasi kidogo tu cha muda kinapaswa kupangwa kuelezana ujumbe muhimu. Kujifunza kwa washiriki walio wengi kutatokea wakati wa mazoezi na muda mwingi unapaswa kupangwa katika hilo. Mazoezi yamebuniwa kuhamasisha kujipima kwa washiriki, mjadala na uchanganuzi.

Wakufunzi wanahamasishwa kujumuisha michezo katika programu yao ya mafunzo. Michezo inaweza kutumiwa kuwafanya watu wawe na bidii; inafurahisha na inaweza kujenga hisia ya msimamo mmoja baina ya kikundi. Michezo pia inaweza kutumika kuligawa kundi zima katika vikundi vidogo kwa ajili ya mazoezi.

Wakufunzi wanapaswa kutoa muda katika programu ya mafunzo kuangalia kwamba washiriki wanaelewa taarifa wanayoelezwa.

[8] Uchaguzi huu unahusisha hatua saba katika Zoezi 10–16 katika zoezi moja fupi. Unaweza kutumika katika programu ya mafunzo kama hakuna muda wa kutosha kujifunza kila hatua kwa kina. Uchaguzi mbadala wa kufanya kila zoezi katika muda tuliopendekeza utachukua angalau saa tano.

## 2.2 UJUMBE MUHIMU NA MAZOEZI

### Zoezi la 1: Ukaribisho na Utambulisho

**Lengo la zoezi**

Kuwakaribisha washiriki, na kujitambulisha mwenyewe na washiriki kujitambulisha kila mmoja.

**Muda unaopendekezwa wa zoezi**

Dakika 30

**Vifaa**

Vibandiko vya majina (hiari)

**Ujumbe muhimu**

- Wakufunzi kumkaribisha kila mmoja kwenye programu ya mafunzo ya FPIC au kipindi cha utambuzi wa jamii.
- Wakufunzi kujitambulisha na asasi zao, na kueleza kwamba wajibu wao ni kufundisha programu ya mafunzo.
- Wakufunzi kueleza kwamba kikundi kitajifunza kuhusu "ridhaa inayotolewa kwa uhuru, kabla na baada ya kupata taaririfa za kutosha" na namna hiyo inavyoweza kusaidia jamii kuwa na sauti kuhusu miradi kama uchimbaji madini, ukataji magogo au mafuta ya mawese, miradi ambayo inaweza kuathiri ardhi yao, utafutaji riziki na mazingira yao.
- Wakufunzi pia wanaweza kutaka kusema kitu ambacho sio wajibu wao; kwa mfano, kwamba hawatahusika katika michakato inayoendelea ya ufanyaji maamuzi ya jamii.

**Maelekezo ya zoezi**

Wakufunzi kumkaribisha kila mmoja kutaja jina lake, anakotoka na kwa nini anahudhuria programu ya mafunzo.

**Vidokezo**

- Fikiria kutumia mchezo kwa utambulisho wa washiriki, tazama Sehemu ya 3.3 kwa ajili ya baadhi ya vifaa katika kutumia michezo.
- Andika kwa nini watu wanasema wanahudhuria programu ya mafunzo — hii itakueleza wanachopendelea na matatizo.
- Kama kuna mradi unaandaliwa karibu na jamii (au kama mradi umependekezwa), na baadhi ya washiriki wanasema hilo ni tatizo, hili linapaswa kutambuliwa na mkufunzi. Mkufunzi anaweza kutaka kuongezea kwamba mradi utajadiliwa wakati wa programu ya mafunzo.

## Zoezi la 2: Makubaliano ya programu ya mafunzo

**Lengo la zoezi**

- Kufikia makubaliano ya namna watu wanavyopaswa kuenenda wakati wa programu ya mafunzo ili kila mmoja ashiriki kikamilifu.
- Kuwahamasisha washiriki kuheshimiana na kusikilizana.

**Muda unaopendekezwa kwa zoezi**

Dakika 30

**Vifaa**

Peni, karatasi kubwa au ubao

**Ujumbe muhimu**

Wakufunzi waseme kwamba wanatarajia kila mshiriki atawaheshimu na kuwasikiliza washiriki wengine wote wakiwemo wanawake, vijana na watu wengine.

**Maelekezo ya zoezi**

- Wakufunzi wawaambie wanafunzi kutaja orodha ya tabia zinazokubalika na njia za kufanya kazi ili kuhakikisha kwamba kila mmoja anaweza kushiriki kikamilifu.
- mawazo hayo yataandikwa kwenye karatasi kubwa au ubao na kuwa "makubaliano" kati ya wakufunzi na washiriki, na baina ya washiriki wenyewe.
- Kama jambo lolote muhimu limeachwa na washiriki, wakufunzi waliongeze katika makubaliano.
- makubaliano yawekwe karibu mbele ya chumba cha mafunzo ili kila mtu aweze kuyaona.

**Vidokezo**

Baadhi ya mifano ya kinachoweza kuwamo kwenye makubaliano ni pamoja na:

- kila mtu (wanawake, wanaume, vijana, wazee) anaweza kushiriki kikamilifu;
- hakuna mtu anayeruhusiwa kuhodhi majadiliano;
- maoni yote yataheshimiwa;
- maoni tofauti yatasikilizwa
- washiriki watanyoosha mkono (au kuonyesha ishara nyingine) kama wanataka kuzungumza, n.k

## Zoezi la 3: Matarajio ya mshiriki

**Lengo la zoezi**

Kuelewa na kuandika matarajio ya washiriki

**Muda unaopendekezwa kwa zoezi**

Dakika 30

**Vifaa**

Peni, karatasi kubwa au ubao

**Ujumbe muhimu**

- Mkufunzi aeleze kwamba ni matarajio yao kuwa kikundi kitajifunza kuhusu "Ridhaa inayotolewa kwa uhuru, kabla na baada ya kupata taarifa za kutosha".
- Wakufunzi pia wanapenda kuelewa matarajio ya washiriki.

**Maelekezo ya zoezi**

- Wakufunzi wawakaribishe washiriki kusema matarajio yao ni yapi kwa mafunzo.
- Matarajio yote (ya wakufunzi na washiriki) yaandikwe kwenye karatasi kubwa au ubao.
- Kisha orodha ya matarajio inaweza kuwekwa karibu na mbele ya chumba cha mafunzo ili kila mmoja ayaone.
- Kukamilisha zoezi hili, wakufunzi wagawe nakala ya programu ya mafunzo kwa kila mshiriki, waeleze kwa kifupi kilichomo kwenye programu na kwamba wakufunzi wanakusudia kuhakikisha matarajio ya washiriki yatafikiwa wakati kikundi kikiwa kinapitia programu.

**Vidokezo**

- Wakufunzi watakuwa na uelewa wa matarajio ya washiriki kutoka katika hatua ya mipango (tazama Sehemu ya 1) na kutokana na utambulisho wa washiriki (Zoezi la 1). Zoezi hili limebuniwa ili kuelewa na kutambua matarajio ya washiriki kwa utaratibu zaidi.
- Zoezi litakuwa likirejewa wakati wote wa programu na wakati wa tathmini ya programu ya mafunzo (Zoezi la 19). Swali muhimu la kuuliza ni: je, matarajio ya washiriki ya mafunzo yamefikiwa?
- Baadhi ya washiriki wanaweza kuwa na matarajio ambayo hayawezi kufikiwa — kwa mfano, kwamba mradi utasimamishwa kwa sababu ya ushiriki wao katika programu ya mafunzo. Wakufunzi wawahamasishe washiriki kuwa na uhalisia kuhusu mafunzo yanachoweza kufanikisha, kutambua kwamba inaweza kuwa vigumu
- kwa maamuzi ya jamii kuheshimiwa na serikali yao au msimamizi wa mradi, lakini kwamba mafunzo ya FPIC yamebuniwa kuisaidia jamii kuelewa na kutetea haki zao hata katika mazingira magumu.

## Zoezi la 4: Kujipima na majadiliano yanayohusu thamani na matumizi ya maliasili zao

**Lengo la zoezi**

- Kuwahamasisha washiriki kujihusisha katika kujipima na majadiliano kuhusu thamani na matumizi ya maliasili zao.
- Kuelewa mitazamo mbalimbali ya wanawake na wanaume.

**Muda unaopendekezwa kwa zoezi**

Dakika 45

**Vifaa**

Nakala za picha za maliasili (tazama Kiambatisho B) — tumia zile picha ambazo ni muhimu tu kwa jamii, karatasi kubwa, peni.

**Ujumbe muhimu**

Kabla ya kujifunza kuhusu FPIC na jinsi inavyoweza kuzisaidia jamii kuwa na sauti kuhusu miradi ambayo inaweza kuathiri ardhi yao au utafutaji riziki, zungumzia kuhusu maliasili katika jamii hii na thamani na matumizi yanayohusiana na maliasili hizo. Hii itaiweka FPIC katika muktadha.

**Maelekezo ya zoezi**

- Unda vikundi vidogo vya watu watano au sita (ukitenga wanawake na wanaume) na kila kikundi kipe picha moja.
- Kiambie kila kikundi kujadili maadili na matumizi wanayoyahusisha na maliasili zinazoonyeshwa kwenye picha.
- Wakufunzi wanaweza kuuliza:
  - Je, maliasili hizi ni muhimu kwa wanajamii? – maliasili hizi zinatumikaje? -- Nani anawajibika kuzisimamia rasilimali hizo?
  - Ni thamani gani inahusishwa na maliasili hizo?
  - Jamii itaathirikaje kama mradi mkubwa utaathiri maliasili hii?
  - Waambie wanawake wafikirie wajibu wao katika jamii, na maarifa yao mahususi na maslahi, na uhusiano kati ya hayo na maliasili zinazowakilishwa na picha hizo. Wanawake wataathirikaje kama mradi mkubwa utaathiri maliasili hizo? Uliza swali hilohilo kwa wanaume, yaani, wataathirikaje na mradi mkubwa ukizingatia wajibu wao, maarifa na maslahi.
- Picha zinaweza kubandikwa kwenye kipande kikubwa cha karatasi na kila kikundi kuombwa kuandika au kuchora picha ili kutoa muhtasari wa mambo makuu kutokana na majadiliano.
- Kila kikundi kitaitwa kutoa ripoti kwenye kundi kubwa.

**Vidokezo**

- Njia moja ya kuunda kikundi kidogo ni kukata kila picha katika vipande vitano au sita (kama fumbo la mlinganisho), gawa vipande kwa washiriki bila kufuata mpangilio, kisha mwambie kila mmoja kuziweka pamoja picha. Hii ina faida ya kumfanya kila mmoja asimame na kuzunguka, na kuunda vikundi vya watu ambao kwa kawaida hawazungumzi. Hata hivyo, uangalifu unatakiwa ili kuhakikisha kwamba wanawake na wanaume wanaunda vikundi tofauti — inaweza kusaidia kutenga kikundi cha wanawake na wanaume kabla ya kugawa vipande vya picha.
- Kama majadiliano yanakwenda taratibu, waambie washiriki kurejea katika maliasili zilizowakilishwa kwa picha na jinsi hizo zinavyohusiana na utafutaji riziki wao, afya, chakula na usalama wa maji, maadili ya kiutamaduni na kiroho na bioanuwai na masuala ya hifadhi.
- Uchaguzi mwingine kwa zoezi hili unaweza kuwa kutoka nje ya chumba cha mafunzo kuangalia jamii na sehemu yake katika mazingira. Watu wanaona nini? Nini thamani na matumizi yapi watu wanahusisha na vitu hivyo?
- Badala yake, wakufunzi wanaweza kuja na picha zao, mabango au video fupi ambazo zitafaa kuanza zoezi hili la kujipima na majadiliano. Zana hizi zinaweza kutolewa na wanajamii wenyewe.

## Zoezi la 5: Kuelewa maana ya Ridhaa inayotolewa kwa "Uhuru"

**Lengo la zoezi**

Kupata uelewa wa kina wa nini maana ya ridhaa inayotolewa kwa "uhuru".

**Muda unaopendekezwa kwa zoezi**

Saa 1 (kiwango cha chini)

**Vifaa**

Rejea kwenye mswada wa Maonyesho ya Jukwaani na maelekezo kwenye Kiambatisho C; watu wanaopenda kuigiza katika mchezo wa Maonyesho ya Jukwaani (hawa wanaweza kuwa wakufunzi au washiriki), "mfanya mzaha", na vifaa na mavazi (hiari).

**Ujumbe muhimu**

- Vipengele vya ridhaa inayotolewa kwa uhuru, kabla na baada ya kupata taarifa za kutosha vinahusiana, na vinapaswa kuweka masharti ya ridhaa ya jamii, kama wataamua kuvitumia. "ridhaa inayotolewa kwa uhuru, kabla na baada ya kupata taarifa za kutosha" yanalinda dhidi ya kuhodhi (au unyonyaji) wa michakato ya ufanyaji maamuzi ya jamii.
- Kila sehemu ya neno ina maana muhimu — katika zoezi hili na mawili yanayofuata, tutaanza kuchunguza na kuelewa maana ya kila moja.
- Ridhaa ya jamii inapaswa kutolewa kwa uhuru tu.
- Uhuru ina maana hakuna kulazimishwa, hakuna kutumia nguvu, hakuna vitisho, hakuna kumilikiwa na hakuna shinikizo kutoka kwa msimamizi wa mradi, serikali au vikundi vingine vyenye maslahi katika mradi kusema ndiyo kwa mradi au kufanya uamuzi kabla jamii haijawa tayari.
- Uhuru pia inamaanisha kila mmoja — wanawake. Wanaume, vijana na wazee — wako huru kushiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi.
- Uhuru inamaanisha kwamba jamii inaweza kusema hapana (au kutotoa ridhaa yake) kwa mradi.

**Zoezi**

- Zoezi hili ni tukio la Maonyesho ya Jukwaani
- Maonyesho ya jukwaani ni aina ya maonyesho ya jamii ya mwingiliano na shirikishi. Ndani yake mgogoro wa jamii au suala la mabishano linaigizwa, pamoja na hadhira husika ikihamasishwa kuingia katika tukio, kubadilisha mmoja wa wahusika na kujaribu kubadilisha vizuri matokeo.
- Maonyesho ya jukwaani ni fursa ya kubainisha na kujaribu mikakati kwa ajili ya mabadiliko katika maisha halisi.
- Wakati wote wa uigizaji hadhira (yaani washiriki) wanakaribishwa kuakisi masuala yaliyowasilishwa katika mchezo na kuhusu maoni ya mabadiliko.
- Kiambatisho C kina taarifa zaidi kuhusu Maonyesho ya jukwaani, ikiwemo wajibu unaotimizwa, maswali ya kuiuliza hadhira, na kitini kwa ajili ya zoezi hili mahususi.



**Vidokezo**

- Kwa kila tukio jaribu kupata angalau uingiliaji kati mara tatu wa hadhira.
- Usihisi kulazimika kuwa na mwisho mzuri mwishoni mwa Mchezo — lengo la Maonyesho ya jukwaani ni mjadala wa jamii na zoezi la mwisho kwa ajili ya hatua ya baadaye.
- Wakati mwingine tunajifunza mengi kutokana na kuingilia kati ambako hakututatui tatizo.
- Usikubali kirahisi suluhisho la "kiini macho", yaani suluhisho ambalo linabadilisha mazingira ya msingi ya mchezo. Kwa mfano, msimamizi wa mradi mwenye hasira anageuzwa kuwa rafiki na mtu mpole. Ingawaje sote tungependa kuona mabadiliko hayo yanatokea, kwa uchanganuzi halisi wa tatizo, inafaa zaidi kujihusisha katika mazingira kama yalivyo.
- Maonyesho ya Jukwaani yanaweza kufaa kama yataendeshwa kama warsha ndogo, ikiruhusu muda wa kujenga uaminifu baina ya washiriki. Kama kuna muda wa kutosha idadi ya michezo ya kuigiza na mazoezi ya kuchangamsha yanaweza kufanywa kabla ya uigizaji wa Maonyesho ya Jukwaani. Kiambatisho C kina baadhi ya michezo.



## Zoezi la 6: Kuelewa maana ya ridhaa inayotolewa "Kabla"

**Lengo la zoezi**

Kupata uelewa wa kina wa maana ya Ridhaa inayotolewa "Kabla"

**Muda unaopendekezwa kwa zoezi**

Saa 1

**Vifaa**

Peni, karatasi kubwa, nakala za igizo kwa kila mshiriki (tazama Kiambatisho D)

**Ujumbe muhimu**

- ridhaa inayotolewa kabla inamaanisha kwamba lazima uombwe ruhusa: -- kabla ya serikali kugawa ardhi kwa matumizi mahususi ya ardhi;
  - kabla ya serikali kuidhinisha mradi mahususi;
  - kabla mradi wa ujenzi kuanza (kwa maneno mengine, kabla ya malori na mabuludoza kuwasili);
  - jamii zipewe muda wa kutosha kujadili taarifa zote zilizotolewa; na
  - jamii zipewe muda wa kutosha kufanya uamuzi kulingana na michakato yao ya ufanyaji maamuzi; kusiwe na shinikizo kufanya uamuzi wa haraka.
- Sio wakati wote jamii zinapewa fursa ya kutoa ridhaa yao kabla. Hata hivyo, zinaweza kujaribu kushawishi mradi wakati mwingine wakati wa mzunguko wa mradi na kujihusisha katika ufanyaji uamuzi wa mradi. Miradi inapitia hasa katika dhana ya mradi (au mawanda na mipango ya awali); mipango yakinifu na ya kina; ujenzi; uendeshaji; na ufungaji au kuacha kutoa huduma.

**Maelekezo ya zoezi**

- Gawanya kundi katika vikudi vidogo vitatu (au kama vikundi hivi vitatu vina watu zaidi ya sita au saba, unda vikundi vya ziada).
- Mpe kila mshiriki nakala ya onyesho (onyesho moja kwa kila kikundi), waambie wasome onyesho kwa pamoja na kisha kurejea kwenye maswali kwa kila onyesho.
- Wakufunzi wakiambie kila kikundi kuandika muhtasari wa majadiliano yao kwenye karatasi.
- Kila kikundi kipewe muda wa kuripoti kwa kundi zima.
- Kama jamii imekuwa katika mazingira yanayofanana na yale yaliyoelezwa katika moja ya maonyesho (hili linaweza kubainishwa wakati wa hatua ya mipango) zingatia sehemu ya mwisho ya zoezi hili kuhusu kuelewa jamii ilifanya nini wakati huo. Ni mawazo gani, mikakati na rasilimali walizotumia kukabiliana na mazingira hayo? Matokeo yalikuwa nini? Je, watafanya chochote tofauti wakati ujao?

**Vidokezo**

- Onyesho la 1 linaeleza mazingira ambapo jamii inagundua kuhusu mradi kabla haujaidhinishwa na serikali; Onyesho la 2 ni kuhusu hali ya mambo mahali ambapo kampuni ya uchimbaji madini imeanza shughuli
- za uchunguzi; na Onyesho la 3 ni kuhusu mazingira ambapo jamii inagundua kuhusu mradi ambao tayari umeshaanza. Lengo la zoezi hili ni kujadili dhana za "kabla", "kwa muda uleule" na "kuchelewa" dhidi ya maana ya ridhaa inayotolewa "kabla" (kama ilivyoelezwa hapo juu katika ujumbe muhimu).
- Wakufunzi wahamasishe majadiliano ya jamii ingefanya nini kama wanajikuta katika mazingira tofauti yaliyoelezwa kwenye maonyesho hayo. Wakufunzi wasisitize kwamba kamwe hakuna kuchelewa sana kushirikiana na msimamizi wa mradi kuwafanya watambue na kusaidia FPIC hata kama kimsingi mradi uliandaliwa bila ya ridhaa ya jamii. Kanuni ni ileile ingawa mwanzo utakuwa tofauti.
- Zoezi hili na baadhi ya mazoezi mengine yanahitaji washiriki kutoa muhtasari wa majadiliano yao kwenye karatasi. Washiriki wahamasishwe kuandika majibu mafupi kwa maswali kuliko kujaribu kuandika majadiliano neno kwa neno. Ni muhimu kwa kila mmoja kushiriki na kuzingatia majadiliano kuliko kulenga zaidi katika kuandika. Hata hivyo, kama viwango vya kujua kusoma na kuandika katika kikundi ni vya chini sana, itakuwa vizuri kutoweka muhtasari wa majadiliano katika maandishi bali badala yake kuzingatia pekee katika majadiliano na kisha muhtasari wa mazungumzo na maoni.

## Zoezi la 7: Kuelewa maana ya rihaa inayotolewa "Baada ya kupata taarifa za kutosha"

**Lengo la zoezi**

Kupata uelewa wa kina wa maana ya ridhaa inayotolewa "baada ya kupata taarifa za kutosha

**Muda unaopendekezwa wa zoezi**

Saa 1

**Vifaa**

Peni, karatasi kubwa

**Ujumbe muhimu**

- Ridhaa inayotolewa baada ya kupata taarifa za kutosha inamaanisha kwamba lazima upewe taarifa zote muhimu kuhusu mradi kufanya uamuzi kuhusu kama unakubaliana au kutokubaliana na mradi:
  - taarifa lazima ziwe katika lugha ambayo unaweza kuielewa na kuwasilishwa katika namna na muundo ambao ni rahisi kuelewa;
  - taarifa lazima ziwe sahihi;
  - lazima upate taarifa zinazojitegemea, sio tu taarifa kutoka kwa msimamizi wa mradi au serikali yako;
  - lazima upewe taarifa kuhusu uchaguzi mwingine kwa ajili ya mradi; na
  - lazima pia upate wataalamu wa masuala ya kisheria na kiufundi, kama utaombwa, kusaidia kutoa uamuzi wako.
- Jamii zinaweza kuomba nakala za nyaraka za mradi ikiwa ni pamoja na zifuatazo: mikataba, leseni au vibali; makubaliano ya mapato; makubaliano ya fidia; ramani za mipaka na rasilimali; tathmini ya athari kwa mazingira na jamii; tafiti za uchaguzi mbadala; kumbukumbu za mikutano ya mashauriano na jamii; mipango ya makazi mapya; maelezo ya namna mradi unavyofuata sheria husika za nchi — wakufunzi wataje nyaraka nyingine ambazo wanafikiri zitakuwa muhimu kwa jamii.

**Maelekezo ya zoezi**

- Unda vikundi vidogo vya watu watano hadi sita na kila kikundi kipe karatasi na peni.
- Kiombe kila kikundi kujadili na kuandika kwenye karatasi maswali waliyonayo kuhusu mradi — washiriki wanataka kujua nini kuhusu mradi?
- Kama kuna mradi maalumu unaoanzishwa au unaofanya shughuli karibu na jamii, waambie washiriki waandike maswali kuhusu mradi.
- Kama hakuna mradi, waambie washiriki waandike baadhi ya maswali kuhusu mradi wa ukataji magogo, uchimbaji madini, uchimbaji mabwawa au mafuta ya mawese — chagua mradi au idadi ya miradi ambayo itakuwa muhimu sana kwa jamii.
- Kiombe kila kikundi kuripoti katika kundi zima.

**Vidokezo**

Mwongozo wa Oxfam wa Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya kupata Taarifa za kutosha wenye orodha ya maswali yanayopendekezwa kumuuliza msimamizi wa mradi. Kama washiriki wanahangaika kuunda maswali yao wenyewe, waelekeze kwenye mwongozo ili waweze kuanza. Wahamasishe washiriki kufikiria maswali kuhusu mradi na nani anauanzisha, mradi unaweza kuwa na athari gani kwa jamii (ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kuhamishwa na makazi mapya) na mashauriano na jamii na hatua za mapatano.

## Zoezi la 8: FPIC na sheria

**Lengo la zoezi**

Kujenga uelewa wa msingi wa sheria za kitaifa na kimataifa, na viwango vya tasnia vinavyohusiana na FPIC.

**Muda unaopendekezwa kwa zoezi**

Saa 1

**Vifaa**

Vitini au projekta/slaidi ambazo zina ujumbe muhimu (hiari)

**Ujumbe muhimu**

Wakufunzi waandae ujumbe muhimu wa kwao wenyewe kwa ajili ya zoezi hili. Jamii zinahitaji kuelewa muktadha wa sheria wa eneo, na viwango mahususi vinavyohusiana na FPIC wanavyoweza kutumia katika mazingira yao. Uwasilishaji wowote ambao hauzingatii mazingira ya nchini unaweza usiwe na manufaa sana.

Wakufunzi wanahitaji kuzingatia:

- Kama mafunzo ni kwa ajili ya wenyeji, kwa hali hiyo Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Wenyeji na Makubaliano ya 169 ya ILO ya Weenyeji na Watu wa makabila ni muhimu. Waalimu waangalie kama serikali inaunga mkono yoyote kati ya hati hizo, na sisitiza sehemu muhimu kwa kila moja (kwa mfano Ibara ya 32(2) ya Azimio).
- Kama mafunzo ni kwa ajili ya watu wasio wenyeji, kwa hali hiyo kurejea katika sheria za haki za binadamu za kimataifa kama vile Makubaliano ya Kimataifa ya Haki za Uchumi, Jamii na Utamaduni yanaweza kuwa
- na manufaa.
- Itakuwaje, kama sheria za nchi, kama zipo, au uamuzi wa mahakama upo kuhusiana na FPIC, upataji wa taarifa, ushiriki katika kufanya maamuzi, n.k. na sheria inamlinda nani (wenyeji tu au raia wote?).
- Ni sera au sheria zipi za taifa zilizopo kuendeleza haki za wanawake ikiwa ni pamoja na kushiriki katika mijadala ya umma na michakato ya kufanya maamuzi.
- Kiwango ambacho sheria za haki za binadamu kimataifa zinaheshimiwa, na sheria za nchi kutekelezwa.
- Kama mahakama, taasisi za taifa za haki za binadamu au vyombo vingine vipo na vinalinda kwa dhati haki za binadamu.

Kama kuna mradi unaandaliwa karibu na jamii, wakufunzi wanapaswa kuelewa nani anauandaa, nani anaugharimia na itakuwaje kama utachochea viwango vyovyote au masharti. Kisha taarifa hizi zinaweza kujumuishwa katika ujumbe muhimu. Kwa kutegemeana na mradi, viwango muhimu vinaweza kujumuisha:

- Sheria za kampuni kuhusiana na FPIC, haki za wenyeji, haki za binadamu, mashauriano na jamii na kusuluhisha malalamiko.
- Kukaa pamoja kuzungumza kuhusu Uendelevu wa Mafuta ya Mawese ambao una masharti mahususi kwa FPIC na una utaratibu wa malalamiko.
- Shirika la Fedha la Kimataifa ambalo Kiwango cha 7 cha Utendaji wake kinahitaji FPIC katika mazingira kadhaa na kina utaratibu wa malalamiko.
- Baraza la Usimamizi wa Misitu ambalo linatambua FPIC

**Maelekezo ya zoezi**

- Wakufunzi waruhusu muda wa maswali na majibu, chemshabongo au zoezi lingine lolote ambalo linawawezesha washiriki kupima maarifa yao na kufafanua mambo ambayo hawayaelewi.
- Uchaguzi mwingine unaweza kuwa kuwaambia washiriki kujadili swali lifuatalo: je, mikakati ya kisheria itafaa kulinda haki na maslahi yao, au mikakati mingine itafaa zaidi?

**Vidokezo**

- Wakufunzi watahitaji kuandaa zoezi hili kama sehemu ya awamu nzima ya mipango ya programu.
- Ujumbe muhimu utakuwa na taarifa za kisheria ambazo zitakuwa za kitaalamu na inaweza kuwa vigumu kuelewa. Wakufunzi wanahitaji kuamua taarifa kiasi gani ni muhimu na kutambua kwamba taarifa nyingi kupita kiasi zinaweza zisiwe za kusaidia. Badala yake, washiriki wanaweza kuvutiwa sana na kutaka taarifa zaidi. Kiasi cha taarifa kinachotakiwa kiamuliwe wakati wa hatua ya kuweka mipango.
- Wakufunzi wakumbuke kwamba ni wenyeji tu ambao wana haki kwa FPIC. Hata hivyo, FPIC inawakilisha maendeleo endelevu ya taratibu nzuri na kwa hiyo, kanuni ambayo serikali na makampuni yanapaswa kuiheshimu wanaposhauriana na kupatana na jamii zote zinazoathirika.
- Wakufunzi waelewe kwamba mara nyingi kunakuwa na upungufu kati ya kile kinachotakiwa na sheria na kama sheria inafuatwa katika uhalisia. Kwa kawaida jamii inabidi zitegemee njia zisizo za kisheria ili kulinda haki na maslahi yao na hili linaweza kuwa kiini cha majadiliano kinachofaa wakati wa zoezi hili.

## Zoezi la 9: Kitu gani kinachotokea katika jamii

**Lengo la zoezi**

- Kufikiria ni kitu gani kinatokea katika jamii.
- Kuimarisha kitu ambacho wamejifunza kuhusu FPIC.

**Muda unaopendekezwa wa zoezi**

Dakika 30

**Vifaa**

Mswali yaliomo katika Kiambatisho E yaliyonakiliwa kwenye karatasi ya kila mtu, karatasi kubwa nne: moja iliyoandikwa "ndiyo", moja iliyoandikwa "hapana", moja iliyoandikwa "kila mtu", moja iliyoandikwa "wachache".

**Ujumbe muhimu**

Sasa tutatafakari kile ambacho kila mtu amejifunza kuhusu FPIC katika muktadha wa kinachotokea katika jamii.

**Maelekezo ya zoezi**

- Weka karatasi iliyoandikwa "ndiyo" upande mmoja wa chumba cha mafunzo na karatasi iliyoandikwa "hapana" upande mwingine wa chumba.
- Waombe watu kumi kujitolea (mmoja kwa kila swali), ukihakikisha kuna idadi sawa ya wanawake na wanaume.
- Liambie kundi zima kujadili kila swali moja baada ya jingine.
- Kwa swali la 1 hadi 5, waulize washiriki kama wanaamini jibu ni ndiyo, hapana au liko katikati. Mtu mwenye swali asogee karibu na "ndiyo", "hapana" au popote katikati kutegemeana na majibu kutoka kwa washiriki wengine.
- Kwa swali la 6 hadi 10, badilisha "ndiyo" na "hapana" na "kila mmoja" na "wachache", kisha waambie washiriki kujadili kama kila mmoja au wanajamii wachache tu wanahusishwa, wanapewa taarifa, wanapata manufaa n.k.
- Hamasisha majadiliano na, kama kuna tofauti za maoni, chunguza hilo — ikiwa ni pamoja na mtazamo wa jinsia: je, wanawake na wanaume wana majibu ya maswali yaliyo sawa au tofauti.

**Vidokezo**

- Zoezi hili linaweza kuangalia miradi iliyopo ndani au karibu na jamii kadri inavyowezekana. Kama hakuna miradi mikubwa kama vile uchimbaji madini au ukataji magogo, iambie jamii kujadili maswali katika muktadha wa mradi mdogo kama vile barabara, kisima cha maji au shule.
- Zoezi hili linapaswa kuwa burudani. Kama kuna tofauti ya maoni miongoni mwa washiriki, mtu mwenye kadi ahamasishwe kusogea (kwa kuruka, kurukaruka au kukimbia) kati ya "ndiyo" na "hapana" kama maendeleo ya mjadala.
- Lengo la zoezi hili sio kukubaliana jibu bali badala yake kujua uzoefu na maoni ya washiriki wote.

**Kabla ya kuanza zoezi la 10, mkufunzi anapaswa kueleza kwamba washiriki sasa watajifunza kuhusu baadhi ya njia za vitendo za kutumia FPIC ili kulinda haki na maslahi yao. Kuna hatua saba (zilizochukuliwa kutoka Mwongozo wa Oxfam wa Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya kupata Taarifa za kutosha ambazo zitazungumziwa katika mazoezi saba yanayofuata.**

**Wakufunzi waeleze kwamba katika maisha halisi hatua hizi sio lazima zifuatwe kwa mpangilio ulioonyeshwa hapa. Kwa mfano, jamii inaweza kuhitaji msaada wa washauri wa kujitegemea mara moja baada ya jamii kujua kwamba mradi unaanzishwa, na majadiliano ndani ya jamii yafanyike mara kwa mara, sio katika pointi moja kwa muda. Na hakika maisha halisi yana utata na kamwe hayafuati seti ya hatua rahisi, iliyofafanuliwa mapema.**

**Badala yake, kwa programu fupi za mafunzo, mkufunzi anaweza kutumia Zoezi la 17. Zoezi la 17 linajumuisha hatua zote saba katika zoezi moja ambalo litachukua saa mbili kukamilika.**

## Activity 10: Step 1 — find out who is developing the project

**Lengo la zoezi**

Kuelewa nani anahusika na kuanzisha miradi mikubwa.

**Muda unaopendekezwa kwa zoezi**

Dakika 30

**Vifaa**

Peni, karatasi kubwa au ubao

**Ujumbe muhimu**

- Unatakiwa kujua nani anapanga mradi ambao unaweza kuathiri jamii yako. Kisha utajua ni watu gani wanaopaswa kutafuta ridhaa yako.
- Wakati mwingine inaweza kuwa vigumu kupata taarifa kuhusu msimamizi wa mradi. Kwa kawaida miradi mikubwa inahusisha mchanganyiko wa maslahi binafsi na ya serikali.
- Kama una matatizo ya kupata taarifa kuhusu mradi, unaweza kupata msaada kutoka kwa asasi nyingine, zikiwemo AZISE za nchini na za kimataifa. Vyombo vya habari, yakiwemo magazeti ya nchini na ya kimataifa na majarida ya viwanda, pia yanaweza kuwa na taarifa kuhusu miradi inayopangwa.
- Wakati mwingine mwendelezaji wa mradi sio wa kutoka nchini mwako. Hii inaweza kuwa vigumu zaidi kuwasiliana nao na unaweza kuhitaji msaada kutoka kwa wengine.

**Maelekezo ya zoezi**

- Kama kuna mradi maalumu unaoanzishwa au unaoendeshwa karibu na jamii waambie washiriki ni nani mwendelezaji mradi. Kisha uliza maswali yakijumuisha:
  - Je, kampuni ni ya kitaifa au ya kimataifa?
  - Je, kampuni inaanzishwa kwa ushirikiano na kampuni zaidi ya moja? Kama ndiyo, nani?
  - Je, kuna kuhusika kokote kwa serikali au kuwa na maslahi katika mradi?
  - nani anagharimia mradi?
  - Je, kuna asasi nyingine yoyote inayohusika?
- Kama washiriki hawajui majibu ya maswali, wahamasishe wajaribu kutafuta baada ya warsha na pendekeza njia wanazoweza kufanya kwa hilo.
- Kama hakuna mradi karibu na jamii, waambie washiriki kubainisha aina ya asasi ambazo zinaweza kuanzisha miradi mikubwa kama vile uchimbaji madini, mabwawa au mashamba ya mawese. Tumia maswali madogo hapo juu kuongoza majadiliano.
- Hitimisha zoezi kwa kuongezea jinsi ilivyo muhimu kwa jamii kuelewa nani anahusika na kuanzisha miradi mikubwa na kwamba hii ni hatua ya kwanza kwa jamii kudai haki yao ya kuamua kinachotokea kwenye ardhi yao.

**Vidokezo**

- Katika matokeo, zoezi hili linawataka washiriki kufanya zoezi la kumfahamu mdau. Wakufunzi wanaweza kutaka kuibua suala la kisiasa au maslahi mengine na uanzishaji mradi. Wakati mwingine makampuni yanajenga tu kile ambacho serikali inataka.
- Mwongozo wa Oxfam wa Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya kupata Taarifa za kutosha ambao unatoa taarifa kuhusu mwanzishaji mradi.
- Hili ni zoezi la kundi kubwa ambapo watu wanaozungumza sana na kujiamini zaidi wanaweza kutawala. Jaribu kuhakikisha kwamba kila mtu anapata fursa ya kuchangia katika majadiliano — mkufunzi awahamasishe watu ambao hawajaongea kuchangia mawazo yao pia

## Zoezi la 11: Hatua ya 2 — kuomba taarifa kutoka kwa mwanzishaji mradi

**Lengo la zoezi**

Kuelewa baadhi ya changamoto katika kupata taarifa na jinsi changamoto hizo zinavyoweza kukabiliwa.

**Muda unaopendekezwa kwa zoezi**

Dakika 45

**Vifaa**

Peni, karatasi kubwa

**Ujumbe muhimu**


- Ni muhimu kujua jinsi mradi unaopendekezwa utakavyoathiri jamii yako. Kisha unaweza kufanya uamuzi kwa kuwa na taarifa muhimu kuhusu:
  - kama unatoa au hutoi ridhaa ;
  - mabadiliko unayotaka katika usanifu wa mradi; na
  - masharti ya awali unayotaka kutimiza kabla ya kufikiria kuukubali mradi.
- Ni muhimu kwa jamii yako kuarifiwa kikamilifu kuhusu mradi, uwezekano wa athari zake na mwanzishaji mradi atafanya nini kuzuia au kupunguza athari mbaya — hii itajumuisha taarifa kuhusu kama jamii itahamishwa na kupewa makazi mapya na mradi.
- Kuomba nakala za tathmini ya athari kwa mazingira na jamii kunaweza kusaidia kuhakikisha wanajamii wote wanapata taarifa za kutosha na kuelewa uwezekano wa kutokea athari. Pia wanajamii waweze kushiriki katika kuandaa tathmini ya athari kwa mazingira na jamii kwa kuwa ni watu ambao wanajua vizuri mazingira ya eneo lao na ambao mradi mkubwa unaweza kuathiri utafutaji riziki wao na mazingira.
- Tarifa lazima zitolewe katika lugha na muundo ambao unaeleweka na jamii.
- Njia nyingine ya kupata taarifa hizi ni kumualika mwanzishaji mradi katika mkutano wa jamii ambapo wanajamii wanaweza kumuuliza maswali kuhusu mradi.
- Jamii inaweza kuomba msaada wa asasi za ndani ili kuwasaidia kuelewa taarifa ambazo zimepatikana.
- Pia unaweza kuuliza moja kwa moja kutoka idara ya serikali inayohusika. Hii inaweza kujumuisha Idara ya Mazingira, Madini, Misitu na Kilimo au Hazina.
- Wakati wa Zoezi 7, washiriki wanaandaa baadhi ya maswali waliyonayo kuhusu mradi — maswali hayo yanaweza kuulizwa kwa mwanzishaji mradi au serikali.
- Sasa kundi litajadili baadhi ya changamoto ambazo zinaweza kuwakabili katika kupata taarifa kuhusu mradi, na jinsi changamoto hizi zinavyoweza kukabiliwa.

**Maelekezo ya zoezi**

- Gawanya kila karatasi katika safu mbili zenye maneno “changamoto” na “utatuzi” yaliyoandikwa juu ya kila safu.
- Wagawe washiriki katika vikundi vidogo vya watu watano au sita.
- Kiambie kila kikundi kujadili changamoto (au vikwazo) wanazoweza kuzipata katika kupata taarifa kuhusu mradi, na namna changamoto hizi zinavyoweza kukabiliwa au ambavyo zimekabiliwa na jamii siku zilizopita (kwa maneno mengine, ni utatuzi upi na jamii ilijaribu kufanya nini kabla).
- Kiambie kila kikundi kutoa muhtasari wa majadiliano yao kwa maandishi kwenye karatasi. Kama viwango vya kutojua kusoma na kuandika viko chini, vikundi vilenge katika majadiliano tu.
- Kiambie kila kikundi kuripoti kwa kundi zima mwishoni mwa zoezi hili kikizingatia katika utatuzi

**Vidokezo**

- Tumia mchezo (tazama Sehemu ya 3.3 kuhusiana na michezo) kuwagawa washiriki katika vikundi vidogo. Hii itakuwa na faida ya kumfanya kila mtu asimame, azunguke na kujichangamsha; na kuunda vikundi vya watu ambao bado hawajafanya kazi pamoja.
- Wakufunzi wanaweza kutaka kusema kwamba mwanzishaji mradi ni chanzo kimoja cha taarifa kuhusu mradi. Pia taarifa zinaweza kupatikana kutoka kwa wengine, vyanzo vya kujitegemea — Zoezi la 14 litalichunguza hili zaidi.



## Zoezi la 12: Hatua ya 3 — fanya majadiliano na jamii

**Lengo la zoezi**

- Kuhakikisha kwamba wanajamii wote wanaweza kushiriki katika majadiliano ya jamii na michakato ya kufanya maamuzi.
- Kuelewa matamanio na mitazamo tofauti ya wanawake na wanaume

**Muda unaopendekezwa wa zoezi**

Saa 1 (kiwango cha chini)

**Vifaa**

Peni, karatasi kubwa (hiari)

**Ujumbe muhimu**

- Mara tu unapowasiliana na mwanzishaji mradi, unapaswa kuanza kujadili mradi kwa kina ndani ya jamii yako.
- Jamii nzima — wanawake, wanaume, vijana na wazee — wapate taarifa za kutosha kuhusu mradi unaopendekezwa.
- Hii itasaidia kuhakikisha kila mmoja anaelewa athari zinazoweza kutokea na faida ambazo mradi unaweza kuwa nazo. Jamii yako iamue kama athari mbaya zinazoweza kutokea zinakubalika ai hazikubaliki, na manufaa gani inayataka katika mradi, kama yapo.
- Ni muhimu sana kuzingatia maoni ya wanajamii wote — kila mmoja ana uwezekano wa kuathiriwa na mradi kwa namna fulani. Jaribu kuhakikisha kwamba wanajamii wote, wakiwemo wanawake, wanaume, vijana na wazee, wanahusishwa katika michakato ya ufanyaji maamuzi. Hii ni kwa sababu mradi mkubwa unamuathiri kila mmoja kwa tofauti.

**Maelekezo ya zoezi**

- Unda vikundi viwili — kikundi kimoja cha wanawake na kingine cha wanaume.
- Kiambie kila kikundi kufikiria kuhusu matamanio au matarajio yao kwa siku zijazo. Waambie wazingatie mitazamo yao matokeo chanya na hasi ya mradi (mradi unaweza kuwa wa uhalisia au wa kufikiria). Kila kikundi pia kiulizwe kama na namna mradi unavyoweza kuchangia katika kufanikisha matamanio yao kwa siku zijazo.
- Kila kikundi kinaweza kutaka kuchora picha kuwakilisha majadiliano. Athari hasi zikoje? Athari chanya zikoje?
- Vikundi viwili vikaribishwe kueleza matamanio na mitazamo yao ya mradi kwa kundi zima. Jadili mambo yanayofanana na kutofautiana, na chunguza sababu za tofauti zozote.
- Wakufunzi wahitimishe zoezi kwa kusisitiza ujumbe kwamba matumaini na mitazamo ya kila mmoja ni muhimu na yana thamani, na kwamba wanajamii wote wahusishwe katika majadiliano ya jamii na michakato ya
- kufanya maamuzi.

**Kidokezo**

- Zoezi hili linalenga mambo ambayo ni muhimu kwa jamii, na hiyo inaweza kuarifu mchakato wa kufanya maamuzi ya siku zijazo na mapatano yoyote na mwanzishaji mradi. Zoezi pia linalenga katika matamanio na mitazamo tofauti kwa wanawake na wanaume.

## Zoezi la 13: hatua ya 4 — mapatano ya jamii na mwanzishaji mradi

**Lengo la zoezi**

Kuelewa kuhusu mapatano na mwanzishaji mradi, na jinsi ugumu katika kufanya hivyo unavyoweza kukabiliwa.

**Muda unaopendekezwa wa zoezi**

Saa 1 (kiwango cha chini)

**Vifaa**

Rejea mswada wa Maonyesho ya Jukwaani na maelekezo katika Kiambatisho C. Watu wanaopenda kuigiza katika Maonyesho ya Jukwaani (hawa wanaweza kuwa wakufunzi au washiriki), "Mfanya mzaha", na vifaa na mavazi (hiari).

**Ujumbe muhimu**

- Kama jamii, una haki ya kuombwa ushauri na kupatana na mwanzishaji mradi.
- Unaweza kushiriki katika kuweka kanuni na masharti ambayo yanashughulikia athari za kiuchumi, kijamii na mazingira za mradi na kupunguza madhara yoyote ambayo yanaweza kusababishwa na mradi.
- Kuongea na waanzishaji haina maana kuwa umetoa idhini ya mradi.
- Weka kumbukumbu zote za mikutano yako yote na mwanzishajii mradi ikiwa ni pamoja na tarehe, waliohudhuria na yaliyojadiliwa,
- Mwanzishajii mradi anapaswa kushauriana na jamii yako na kupata ridhaa inayotolewa kwa uhuru, kabla na baada ya kupata taarifa za kutosha katika hatua za mwanzo za mipango ya mradi na kabla ya kila hatua mpya ya mradi.
- Kama kuna uwezekano wa utoaji wa makazi mapya kwa jamii, lazima kuwe na mapatano ya kanuni na masharti na kampuni na kuwekwa katika maandishi kabla ya uamuzi wa mwisho kufanyika.
- Ujenzi wa miradi mikubwa ya maendeleo kwa kawaida inaleta manufaa makubwa ya kifedha kwa mwendelezaji mradi na serikali. Bahati mbaya, mara nyingi jamii za wenyeji hazipewi fursa kushirikiana katika manufaa ya kifedha na mengine.
- Kuanza kutumia tratibu za "kugawana faida" kunaweza kuhakikisha jamii zinazoathiriwa na mradi kupata baadhi ya manufaa kutokana na mradi — jamii inaweza kupatana na mwanzishaji mradi (na huenda na serikali yako pia) kuhusu manufaa.
- Ni muhimu kwamba wanajamii wako wote— wanawake, wanaume, vijana na wazee — wanahusishwa katika mapatano na mwanzishaji mradi na sio na viongozi wachache tu au "wasomi" ambao wanaweza kuwa wanapendelea kuongeza manufaa yao binafsi kwa gharama ya jamii nzima.
- Kupatana na mwanzishaji mradi inaweza kuwa vigumu — zoezi linaonyesha baadhi ya ugumu huo.

**Maelekezo ya zoezi**

- Zoezi hili ni tukio jingine la Maonyesho ya Jukwaani
- Kiambatisho C kina mswada wa zoezi hili.

**Vidokezo**

- Jaribu tena kupata angalau uingiliaji kati wa hadhira mara tatu kwa kila onyesho.
- Kumbuka kwamba hupaswi kuhisi kulazimika kuwa na mwisho wenye furaha mwishoni mwa Maonyesho ya Jukwaani— lengo la Maonyesho ya jukwaani ni mjadala wa jamii na mazoezi kwa ajili ya hatua ya siku zijazo. Wakati mwingine tunajifunza mengi kutokana na uingiliaji kati ambao hautatui tatizo.
- Washiriki wanapaswa kuelewa Maonyesho ya Jukwaani baada ya kuyatumia katika Zoezi la 5. Kunaweza kusiwe na haja ya michezo ya kujichangamsha au maelekezo zaidi kwa zoezi hili.
- Jaribu kuhamasisha watu ambao hawakushiriki katika zoezi la kwanza la Maonyesho ya Jukwaani ambao walikuwa kama "watazamaji" kushiriki safari hii.

## Zoezi la 14: Hatua ya 5 — tafuta ushauri huru

**Lengo la zoezi**

Kuelewa nani anaweza kuipa jamii ushauri huru

**Muda unaopendekezwa wa zoezi**

Dakika 30

**Vifaa**

Peni, karatasi kubwa au ubao

**Ujumbe muhimu**

- Kupatana na mwanzishaji mradi inaweza kuwa vigumu, wakati zoezi la awali linachunguzwa. Wakati mwingine mwanzishaji i mradi hujaribu kuepuka kuzihusisha jamii na masuala yanayohusishwa yanaweza kuwa magumu.
- Unaweza kujaribu kupata ushauri na utaalamu binafsi kusaidia kuelewa athari za mradi unaopendekezwa.
- Kumbuka kwamba uamuzi wako unapaswa kuwa uamuzi wenye taarifa za kutosha. Ni muhimu kutotegemea tu taarifa unazopewa na mwanzishaji mradi. Waanzishaji mradi wanaweza kujaribu kufanya mradi uonekane
- unavutia kwa jamii zilizoathirika ili kupata ridhaa yao na wanaweza wasikupe taarifa zote kuhusu mradi — hasa hatari na athari hasi.
- Taarifa kutoka vyanzo vingine zitahakikisha unaelewa kikamilifu athari za mradi za muda mfupi na mrefu, na haki zako ni zipi.
- Taarifa hizi pia zinaweza kukusaidia kuandaa maswali zaidi kwa ajili ya mwanzishaji mradi kuhusu namna wanavyopanga kushughulikia hatari na kuzuia athari hasi.

**Maelekezo ya zoezi**

- Waambie washiriki wapendekeze majina ya watu au asasi ambazo zinaweza kuzipa jamii zao ushauri huru, au ambao wamefanya hivyo siku za nyuma kwa ajili ya jamii. Taja ni nani jamii inaweza kumuona au kuwa na uhusiano naye — hii itasaidia kwa mipango yoyote ya utekelezaji ya baadaye.
- Yaandike hayo kwenye karatasi.

**Vidokezo**

- Kama sehemu ya matayarisho yao, wakufunzi wanaweza kuandaa orodha ya asasi za nchini ambazo zinaweza kutoa msaada kwa jamii — wakufunzi waangalie asasi hizo zinatoa huduma gani au ushauri zinazoweza kutoa, na kama zinatolewa bure au kwa gharama.
- Kama ushauri binafsi unagharimu fedha, wakufunzi wanaweza kuuliza jinsi fedha hizo zitakavyopatikana au kupendekeza vyanzo mbadala vya ushauri.
- Mwongozo wa Oxfam wa ridhaa inayotolewa kwa uhuru, kabla na baada ya kupata taarifa za kutosha, una orodha ya asasi ambazo zinaweza kuzisaidia jamii — hata hivyo, zilizo nyingi ni asasi za kimataifa na kwa hiyo zinaweza zisiwe na msaada sana kama asasi za nchini.

## Zoezi la 15: Hatua ya 6 — kufanya maamuzi kama jamii

**Lengo la zoezi**

- Kuelewa michakato ya jamii ya ufanyaji maamuzi.
- Kuhakikisha mikakati ya ufanyaji maamuzi ya baadaye inajumuisha wanajamii wote, ikiwa ni pamoja na wanawake, vijana na wazee.

**Muda unaopendekezwa wa zoezi**

Saa 1 (kiwango cha chini)

**Vifaa**

Peni, karatasi kubwa

**Ujumbe muhimu**

- Ridhaa inayotolewa kwa uhuru, kabla na baada ya kupata taarifa za kutosha ni haki ya pamoja — sio haki ya mtu mmoja. Kwa hiyo, jamii lazima ifanye uamuzi kwa pamoja.
- Ufanyaji uamuzi wa jamii utahusisha tathmini ya athari chanya na athari hasi za mradi na uamuzi wa manufaa ya jumla kwa jamii.
- Wanajamii wote — wanawake, wanaume, vijana na wazee — lazima wahusishwe katika michakato ya ufanyaji maamuzi.
- Kama jamii yako inaamini kwamba mradi hautafaa kwa jamii, unaweza kusema "hapana" — au kwa maneno mengine, usitoe ridhaa yako — kwa mradi huo. Badala yake, jamii inaweza kutaka mradi uendelee lakini kama tu masharti kadhaa yatatimizwa — masharti haya yanaweza kuhusiana na manufaa ya jamii na kupunguza madhara au athari hasi.
- Mradi unaweza kuendelea tu kama ridhaa ya jamii imetolewa kwa serikali na mwanzishaji mradi.
- Kama jamii inatoa ridhaa yake kwa mwanzishaji mradi, masharti ambapo ridhaa inatolewa yanapaswa kuandikwa ila kila mmoja awe na uelewa mzuri wa masharti ya ridhaa ni yapi.

**Maelekezo ya zoezi**

- Unda vikundi vya wanawake, wanaume, vijana wa kike na vijana wa kiume.
  - Kiombe kila kikundi kuangalia namna kwa sasa wanavyojihusisha katika michakato ya jamii ya kufanya maamuzi
  - Ni masuala gani yanahusika na kufanya maamuzi?
  - Maamuzi hayo yanafanywaje?
  - Je, kuna masuala ambayo hawawezi kuyafanyia maamuzi?
  - kama hawahusishwi katika majadiliano ya jamii na michakato ya ufanyaji maamuzi, au kama wanaweza tu kushiriki katika namna fulani, kwa nini ni hivyo?
- Kisha kiambie kila kikundi kuangalia namna ambavyo wangependa kuhusishwa katika hatua yoyote ya kufanya uamuzi siku zijazo kuhusu miradi ya karibu na jamii yao?
- Ni vikwazo vipi vitahitaji kukabiliwa ili kuwezesha ushiriki wao katika michakato ya ufanyaji maamuzi?
- Waambie warudi katika kundi moja. Kiambie kila kikundi kiseme kingependa kuhusishwaje katika hatua yoyote ya kufanya maamuzi siku zijazo kuhusu miradi mikubwa. Hamasisha majadiliano miongoni mwa kundi zima.

**Vidokezo**

- Zoezi hili lisijaribu kutoa uamuzi wa jamii kuhusu mradi wowote ambao unaanzishwa jirani (kama kuna mradi huo). Kutoa uamuzi kwa jamii kuna ugumu na kutachukua muda — muda mrefu zaidi kuliko ambavyo unaoruhusiwa na zoezi hili. Kumbuka hili ni somo la mafunzo sio somo la kufanya uamuzi.
- Badala yake zoezi limebuniwa kuhamasisha kufikiria na kujadili namna maamuzi yanavyofanywa katika jamii, na namna ya michakato ya kufanya maamuzi ya siku zijazo inavyoweza kujumuisha wanajamii wote.
- Mara nyingi wanawake katika jamii nyingi wanakabiliwa na vikwazo vingi vya kushiriki katika michakato ya jamii (na kaya) ya kufanya maamuzi. Kwa hiyo, wakufunzi watahitaji kusimamia zoezi hili kwa makini. Majadiliano kuhusu namna ya kuhusisha wanawake katika michakato ya kufanya maamuzi yanaweza kuwa na matokeo hasi kwa wanawake katika kundi. Kuzungumza na vikundi vya wanawake kutoka katika jamii wakati wa mipango ya programu ya mafunzo ya FPIC kutamsaidia mkufunzi kuelewa na kuepuka hatari hizo.
- Kama kuna kukataa kokote kwa upande wa baadhi ya washiriki kuunga mkono uhusishwaji wa wanajamii wote (kwa mfano, ushiriki wa wanawake au vijana), hili linapaswa kupingwa na mkufunzi. Mkufunzi anaweza kuwauliza washiriki mifano ya wajibu wa kimila wa kufanya maamuzi kwa wanawake. Pia mkufunzi anaweza kuuliza mifano ya namna wanawake na wanaume wanavyoshirikiana katika lengo au kazi ya pamoja, na kujadili namna mchango wa wanawake na wanaume unavyothaminiwa kwa usawa. Pia wakufunzi waweke wazi kwamba FPIC na haki ya kufanya uamuzi kwa mshiriki ni haki ya watu wote — sio wanaume tu, au baadhi wa wanaume.
- Majadiliano ya kundi zima ni muhimu sana kwa kuwa yanaruhusu mitazamo tofauti kusikilizwa na huenda matokeo ya makubaliano kwamba michakato ya kufanya maamuzi ya siku zijazo yanapaswa kujumuisha wanajamii wote.

## Zoezi la 16: Hatua ya 7 — mawasiliano yanayoendelea na mwanzishaji mradi

**Lengo la zoezi**

- Kuelewa kwamba FPIC ni hatua inayoendelea.
- Kujifunza kuhusu mawasiliano yanayoendelea na mwanzishaji mradi.

**Muda unaopendekezwa wa mradi**

Dakika 30

**Key messages**

- Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru,Kabla na Baada ya kupata Taarifa za kutosha ni mchakato unaoendelea. Miradi mikubwa ya maendeleo inachukua miaka mingi kupanga na kisha kuanza, na inaweza kuathiri jamii yako kwa miaka kadhaa au hata vizazi vingi.
- FPIC sio mchakato wa "mara moja tu", ni mchakato unaoendelea. Hii ina maana mjadala wa kawaida na makubaliano kati ya mwanzishaji mradi na jamii zinazoathirika ni kitendo kizuri. Majadiliano hayo ya mara kwa mara ni njia moja ya kuhakikisha kwamba jamii zinapata taarifa wakati wa kipindi cha mradi na zinaweza kushiriki katika michakato endelevu ya kufanya maamuzi.
- Mwanzishaji mradi ahakikishe kwamba mnaarifiwa mara kwa mara kuhusu mradi. Lazima mpewe nafasi ya kuuliza mawali na kueleza matatizo. FPIC lazima iheshimiwe wakati wote wa mchakato. Hujachelewa kushirikiana na mwanzishaji mradi kuwafanya watambua FPIC.
- Kimsingi miradi mikubwa inapita katika hatua:
  - dhana ya mradi (au mawanda na mipango ya awali)
  - mipango yakinifu na ya kina
  - ujenzi
  - uendeshaji
  - ufungaji au kuacha kutumika.
- Wawakilishi wa jamii wafuatilie mradi, kama mradi unaendelea. Ni muhimu kwa jamii kufuatilia kama mwanzishaji anatimiza ahadi zake.
- Unaweza kutaka kuanzisha jukwaa la kudumu la jamii na mwanzishaji mradi kwa ajili ya mawasiliano ya mara kwa mara. Jukwa hili linaweza pia kutumiwa kushughulikia matatizo au malalamiko unayoweza kuwa nayo kuhusu mradi. Jukwaa hili lijumuishe wanawake, wanaume, vijana na wazee kutoka katika jamii.

**Maelekezo ya zoezi**

- Hakuna zoezi; badala yake wakufunzi wanaweza kutaka kutoa "muhtasari" wa haraka wa hatua saba kabla ya kuingia katika Zoezi la 18, ambalo ni kufikiria kwa jamii na zoezi la kupanga utekelezaji.

**Zoezi la 17 linahusisha hatua saba katika Zoezi la 10 hadi 16 katika zoezi moja fupi ambalo litachukua takribani saa mbili kukamilika. Fanya hivyo wakati una muda mfupi.**

**Wakufunzi waeleze kwamba katika maisha halisia hatua hizi sio lazima kufuatwa kwa mpangilio uliomo humu. Kwa mfano, jamii inaweza kutaka msaada wa washauri wa kujitegemea mara moja baada ya jamii kujua kwamba mradi unaanzishwa, na majadiliano ndani ya jamii yafanyike mara kwa mara, sio mara moja moja. Na kwa hakika maisha halisi yana utata na kamwe hayafuati seti ya hatua rahisi, zinazoelezwa kabla.**

## Zoezi la 17: Hatua ya 1 hadi 7 — Kujifunza kuhusu Hatua ya 1–7 (Uchaguzi B)

**Lengo la zoezi**

Kuelewa baadhi ya njia za vitendo za kutumia FPIC ili kulinda haki na maslahi ya jamii.

**Muda unaopendekezwa wa zoezi**

Saa 2

**Vifaa**

Peni, vipande saba vya karatasi, Mwongozo wa Oxfam wa Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya kupata Taarifa za kutosha au kadi za Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya kupata Taarifa za kutosha.

**Ujumbe muhimu**

- Hatua saba zifuatazo ndizo njia zinazopendekezwa ili kutumia FPIC kulinda haki na maslahi ya jamii.
- Hatua saba zinaweza kusaidia kuhakikisha kwamba kama jamii inatoa ridhaa yake kwa mradi kwamba ridhaa hiyo itakuwa inatolewa kwa "Uhuru", "Kabla" na " Baada ya kupata Taarifa za kutosha".
- Hizi ni hatua saba:
  - Hatua ya 1: tafuta nani anaandaa mradi
  - Hatua ya 2: omba taarifa kwa mwendelezaji mradi
  - Hatua ya 3: fanya majadiliano na jamii
  - Hatua ya 4: mapatano ya jamii na mwanzishaji mradi
  - Hatua ya 5: tafuta ushauri wa kujitegemea
  - Hatua ya 6: fanya maamuzi kama jamii
  - Hatua ya 7: mawasiliano yanayoendelea na mwanzishaji mradi.

**Maelekezo ya zoezi**

- Gawanya kila karatasi katika safu mbili zenye maneno "changamoto" na "utatuzi" yaliyoandikwa juu katika kila safu.
- Unda vikundi saba, kila kikundi kipe hatua ya kujadili na kila kikundi kipe peni na karatasi kubwa.
- Kwanza kiambie kila kikundi kusoma kuhusu hatua yao — lirejeshe kundi katika ukurasa husika wa Mwongozo wa Oxfam wa ridhaa inayotolewa kwa uhuru, kabla na baada ya kupata taarifa za kutosha au kadi za ridhaa inayotolewa kwa uhuru, kabla na baada ya kupata taarifa za kutosha.
- Kiambie kila kikundi kujadili changamoto (au vikwazo) wanavyoweza kukabiliana navyo katika hatua hii, na jinsi changamoto hizo zinavyoweza kukabiliwa au ambavyo zimekabiliwa na jamii siku zilizopita (kwa maneno mengine, ni utatuzi gani na jamii imejaribu kufanya nini kabla).
- Lambie jamii kuangalia uzoefu wao. Ni mawazo gani, mikakati na rasilimali ambazo jamii imetumia kukabiliana na baadhi ya changamoto zilizotajwa katika zoezi? Matokeo yalikuwaje?
- Kiambie kila kikundi kuandika muhtasari wa majadiliano yao kwenye karatasi.
- Kiambie kila kikundi kuripoti katika kundi zima.
- Toa muda kwa kundi zima kujadili walichojifunza.

**Vidokezo**

- Kama idadi ya watu wanaoshiriki katika mafunzo ni ndogo, baadhi ya hatua zinaweza kuunganishwa pamoja na kila kikundi kuombwa kukamilisha zoezi kwa hatua mbili au tatu.
- Wakufunzi pia wanaweza kutumia picha ambazo zinawakilisha kila hatua kama kichocheo cha majadiliano—picha hizi zinaweza kupatikana kwenye Mwongozo wa ridhaa inayotolewa kwa uhuru, kabla na baada ya kupata taarifa za kutosha. Hii inaweza kuwa bora kuliko kusoma kuhusu kila hatua, hasa wakati washiriki wakiwa wana elimu ndogo.

## Zoezi la 18: Mawazo ya mshiriki na mpango wa utekelezaji wa jamii

**Lengo la zoezi**

Kuchochea mawazo na majadiliano ya hatua zinazoweza kuchukuliwa na jamii kutokana na mafunzo ya FPIC.

**Muda unaopendekezwa wa zoezi**

Saa 1

**Vifaa**

Peni, karatasi kubwa tatu zilizoandikwa "mwezi ujao", "miezi mitatu ijayo" na "mwaka huu"

**Ujumbe muhimu**

- Kundi limejifunza kuhusu FPIC na jinsi inavyoweza kulinda haki na maslahi ya jamii.
- Lengo la zoezi hili ni kufikiria kuhusu ni hatua gani jamii inaweza kutaka kuchukua sasa wakati inajua zaidi kuhusu FPIC, na kuanza mchakato wa kuandaa mpango wa utekelezaji wa jamii.
- Hatutakuwa na majibu yote leo lakini tutaanza. Jamii inaweza kutaka kuandaa mikutano mingine ya jamii ili kuendelea na mchakato wa mipango ya utekelezaji.

**Malekezo ya zoezi**

- Waambie washiriki wote wafikirie kuhusu walichojifunza wakati wa programu ya mafunzo ya FPIC. Kama wanapenda wanaweza kuandika, au kujadili na mtu mmoja au wawili wengine. Ruhusu takribani dakika tano kwa hilo.
- Unda vikundi vya watu watano hadi sita — hivi vinaweza kuwa vikundi vya wanawake na wanaume pamoja au vikundi tofauti kwa kila jinsi.
- Kiombe kila kikundi kufikiria kuhusu ni hatua gani wangependa jamii kuchukua kwa pamoja:
  - mwezi unaofuata
  - katika miezi mtatu ijayo – katika mwaka unaokuja.
- Kiombe kila kikundi kuripoti kwa kundi zima, kuandika mawazo yao kwenye karatasi tatu.
- Toa muda kwa kundi zima kujadili mawazo hayo, namna wengine katika jamii ambao hawajapata mafunzo haya wanavyoweza kushiriki, na jnsi baadhi ya mawazo haya yanavyoweza kuendelezwa.

**Kidokezo**

Hakikisha zoezi hili linarekodiwa vizuri na kwamba kuna umiliki wa mazao.

## Zoezi la 19: tathmini ya programu ya mafunzo na kufunga

**Lengo la zoezi**

Kutathmini programu ya mafunzo ya FPIC.

**Muda unaopendekezwa kwa zoezi**

Dakika 30

**Vifaa**

Peni, fotokopi za karatasi kwa kila mshiriki na/au karatasi kubwa.

**Ujumbe muhimu**

- Programu ya maunzo ya FPIC inakaribia kuisha. Kabla ya kumaliza wakufunzi wanataka:
  - kuelewa kama washiriki wameongeza uelewa wao wa FPIC kutokana na kushiriki katika programu ya mafunzo;
  - kuelewa kama matarajio ya washiriki kwa mafunzo yamefikiwa (rejea nyuma kwa kilichojadiliwa katika Zoezi la 3); na
  - kuboresha na kuongeza programu za mafunzo za siku zijazo.
- Wakufunzi pia wanataka kusheherekea mafanikio ya programu ya mafunzo na washiriki.

**Maelekezo ya zoezi**

- Sehemu ya 3.2 ina idadi ya vifaa vya tathmini au wakufunzi wanaweza kuandaa za kwao.
- Chagua kifaa kimoja au viwili vya tathmini ambavyo unafikiri vitafaa zaidi na waambie washiriki kujaza fomu ya tathmini au kushiriki katika zoezi la tathmini.
- Funga mkutano kwa kumshukuru kila mmoja kwa kushiriki kwao na wapongeze kwa programu ya mafunzo ya FPIC yenye mafanikio

**Vidokezo**

- Toa muda kwa washiriki kukamilisha tathmini — hakikisha unakusanya fomu za tathmini.
- Fikiria jinsi utakavyotumia taarifa zilizokusanywa kupitia mchakato wa tathmini ili kuboresha programu za mafunzo za FPIC za siku zijazo.
- Wakufunzi wanaweza kutaka kumpa kila mshiriki cheti kutambua kwamba wameshiriki katika programu hii ya mafunzo.

# 3 ZANA NYINGINE

## 3.1 VIDOKEZO KWA WAKUFUNZI

Hapa kuna baadhi ya vidokezo zaidi kwa wakufunzi:

- Toa maelekezo ya wazi ikiwa ni pamoja na ni muda gani washiriki wanao kwa mazoezi na usizidishe muda.
- Kama unauliza swali la kikundi, uliza swali moja kwa zamu.
- Jaribu kadri ya uwezo wako kuuliza maswali ambayo yanawaruhusu washiriki kuamua au kueleza kitu fulani kuliko kuuliza maswali ambayo majibu yake yatakuwa ndiyo au hapana.
- Muhamasishe kila mmoja kushiriki — hii itahitaji kuelekeza maswali kwa watu ambao hawajaongea bado, au kuwaambia kuripoti kuhusu majadiliano ya vikundi vidogo kwenye kundi kubwa. Jaribu kuepuka mazingira ambapo watu wanaoongea sana na wenye kujiamini zaidi kutawala.
- Jaribu kuchanganya vikundi kwa kila zoezi ili washiriki wapate fursa ya kusikiliza na kubadilishana mawazo yao na watu tofauti wakati wa programu ya mafunzo.
- Toa taarifa sahihi — kama hujui jibu la swali ni sawa kukiri hivyo na kama unaweza, ahidi kutafuta jibu ili kuwaambia washiriki baadaye.
- Kama mshiriki atatoa taarifa yoyote ambayo unajua sio sahihi, msahihishe — tambua kwamba taarifa sio sawa na maoni, ni sawa kama watu wana maoni ambayo hukubaliani nayo.
- Jaribu kuifanya programu ya mafunzo kuhama kutoka zoezi moja hadi jingine ili programu nzima ikamilike — wakati majadiliano ya papo hapo yanaweza kuwa ya kuvutia sana nay a maana kwa washiriki, hili liwianishwe na thamani ambayo kila mmoja atapata kwa kumaliza programu nzima katika muda uliopangwa.
- Toa muda wa kuendelea kufikiria na "kagua" na washiriki wakati wa programu ya mafunzo — hii inahakikisha kama washiriki wanaelewa taarifa zinazojadiliwa, na kama programu itatolewa katika namna ambayo inafaa kwa washiriki. Kama haifai, programu inaweza kubadilishwa ili washiriki waelewe na kushiriki kikamilifu.

Sio wajibu wa wakufunzi kutatua mara moja (au kujaribu kutatua) mgogoro au kutoelewana kati ya wanajamii. Hata hivyo, kama mgogoro mkubwa utazuka au kutokubaliana wakati wa programu ya mafunzo, wakufunzi wanaweza kutakiwa kuingilia kati. Madhumuni ya kuingilia kati yanapaswa kuruhusu programu ya mafunzo kuendelea, kuliko kujaribu kusuluhisha mgogoro. .

Wakufunzi wanaweza:

- Kutambua kwamba baadhi ya washiriki hawakubaliani.
- Kama ni lazima, tambua kwamba kutokubaliana kunakatiza programu ya mafunzo.
- Wakumbushe washiriki kwamba lengo la programu ni kwa kila mmoja kujifunza kuhusu FPIC.
- Pendekeza kwamba ni vizuri kutoelewana kutatuliwe wakati na mahali pengine.
- Omba kwamba watu wasiokubaliana kuacha kubishana na kwamba kundi zima liweke mkazo wake katika zoezi la wakati huo.

## 3.2 KUTATHMINI PROGRAMU YAKO YA MAFUNZO YA FPIC

Tathmini ni upimaji wa thamani ya programu ya mafunzo kwa kuzingatia ubunifu wake, uwasilishaji na athari. Wakufunzi wafanye tathmini kwa kila programu ya mafunzo ya FPIC.

Tathmini inawaruhusu wakufunzi:

- Kuelewa kama washiriki wameongeza uelewa wao wa FPIC na kujisikia huru kuchukua hatua kutokana na programu ya mafunzo.
- Boresha na rekebisha programu za mafunzo za baadaye, kama ni muhimu, kwa kuzingatia masomo yaliyofundishwa.
- Wajibika kwa wahisani au wagharimiaji (kama mafunzo yanasaidiwa na wahisani) na kwa jamii na wadau wengine.

Tathmini ifanyike mwishoni mwa programu na izingatie maoni ya washiriki, na fikra za wakufunzi. Maoni kutoka kwa washiriki yakusanywe kwa tofauti kwa wanawake na wanaume kwa kuwa uzoefu wao wa mafunzo unaweza kuwa tofauti.

Baadhi ya mifano ya maswali ya tathmini ya kuuliza na zana ambazo zinaweza kutumiwa zinafuata. Baadhi ya zana zinafaa vizuri katika mazingira ambayo viwango vya kutojua kusoma na kuandika ni vikubwa. Zana mbili au zaidi zinaweza kutumiwa kutathmini programu ya mafunzo — kila zana inaweza kutoa taarifa zinazotofautiana kidogo na, kama zinatumika kwa pamoja, zitawapa wakufunzi majibu ya kueleweka kutoka kwa washiriki.

Baadhi ya maswali ya kuwauliza washiriki ni pamoja na:

- Je, matarajio yako ya mafunzo yamefikiwa?
- Je, uliweza kushiriki kikamilifu katika programu ya mafunzo?
- Ni kitu gani ulikipenda kuhusu programu ya mafunzo?
- Kuna kitu chochote hukukipenda au unafikiri kingeweza kufanywa tofauti kwa siku za baadaye?
- Unaelewa FPIC ni nini?
- Je, unahisi kujiamini zaidi kutetea haki na maslahi yako?
- Je, unahisi kujiamini zaidi kushiriki katika michakato ya kufanya maamuzi ya jamii?
- Je, unaamini kwamba michakato ya ufanyaji maamuzi ya jamii ya siku zijazo itajumuisha wanajamii wote?
- Je, unajiamini zaidi kudai kwamba makampuni na serikali yako wanakuhusisha katika michakato ya kufanya maamuzi inayohusiana na mradi?
- Utachukua hatua gani kutokana na kushiriki katika programu ya mafunzo ya FPIC?

Tathmini inaweza kufanyika kwa kutumia fomu ya tathmini ambayo kila mshiriki anaijaza. Mfano wa fomu ya tathmini unaweza kupatikana katika Kiambatisho F, ambayo inaweza kutolewa fotokopi kwa ajili ya washiriki kuijaza. Kiambatisho F pia kina baadhi ya maswali yanayopendekezwa kuongoza tathmini binafsi kwa wakufunzi.

Tathmini inaweza kufanyika kama zoezi la "kabla/baada". Hili linamsaidia mkufunzi kuelewa jinsi maarifa na uzoefu wa washiriki umebadilika kutokana na kushiriki kwenye programu ya mafunzo. Kwa mfano, wakufunzi wanaweza kuuliza washiriki walielewa nini kuhusu FPIC kabla ya mafunzo, na wameelewa nini mwishoni. Au, washiriki walijiamini vipi kutetea haki na maslahi yao kabla ya mafunzo na wanajisikiaje kujiamini baada ya mafunzo. Zoezi hili linaweza kufanyika kama zoezi la mtu mmoja pale ambapo kila mshiriki anajaza fomu ya tathmini. Badala yake, linaweza kufanyika kama zoezi la kikundi ambapo washiriki wanaweka majibu yao kwenye maswali ya kabla/baada kwenye karatasi kubwa. Karatasi inaweza kuandaliwa mapema pamoja na maswali yaliyoandikwa na kuachwa nafasi ya kuweka majibu.

Zana nyingine ya tathmini ambayo wakufunzi wangetaka kutumia ni "mduara wa matokeo". Zana inatoa tathmini ya haraka ya kuona ya programu ya mafunzo na inaweza kutumika kama sehemu ya zoezi la tathmini ya kikundi. Zana hii ya tathmini inahitaji karatasi kubwa (moja kwa kila swali) ambayo imewekwa mduara. Washiriki wanaambiwa kuweka jibu lao kwenye swali la tathmini mahali fulani kwenye mduara — kadri inavyokaribia katikati ya mduara ndivyo jibu linavyokuwa chanya. Kwa mfano, wakufunzi wanaweza kuwauliza washiriki kama matarajio yao ya mafunzo yalifikiwa. Washiriki wanaohisi kwamba matarajio yao yalifikiwa wanapaswa kuweka alama karibu na katikati ya mduara, na wale wanaohisi matarajio yao hayakufikiwa waweke alama karibu na ukingo.

Wakufunzi wanahitaji kufikiria kwa makini kuhusu wanachotaka kujifunza kupitia tathmini, na kisha kuamua ni maswali gani wanapaswa kuuliza na zana zipi za tathmini zinaweza kuwa za manufaa zaidi.



## 3.3 VIFAA VINGINE VYA MAFUNZO

Kitabu cha Mwongozo wa Mafunzo: Kuweka Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya kupata taarifa za kutosha katika Vitendo REDD+ Initiatives, RECOFTC — Kituo cha Watu na Misitu, Taasisi ya Mikakati ya Dunia ya Mazingira (IGES) na Shirika la Norwe la Ushirikiano wa Maendeleo (Norad): www.recoftc.org/site/resources/Putting-Free-Prior-and-Informed-Consent-into-Practice-in-REDD-Initiatives.php

Kitabu cha Mwongozo kuhusu Free, Prior and Informed Consent (FPIC) in REDD+ kwa Wenyeji, Mkataba wa Asia wa Wenyeji (AIPP) and International Work Group for Indigenous Affairs (IWGIA): ccmin.aippnet.org/ourpublications/article/1041/FPIC-Manual-web2.pdf

Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Wenyeji (UNDRIP) la ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya kupata taarifa za kutosha (FPIC): aippnet.org/ docs/pub/FPIC-info-poster.jpg



Our Ancestral Lands ni filamu fupi ya vikatuni inayotoa utangulizi wa UNDRIP, Azimio la

Umoja wa Mataifa la Haki za Wenyeji: iva.aippnet.org/our-ancestral-lands-video

Misingi ya Uhusishaji wa Jamii, David K. Deng, Chama cha Sheria Sudani Kusini: www.mokoro.co.uk/files/13/file/lria/SSLS_Community%20Engagement%20Fundamentals.pdf

Mafunzo kwa mabadiliko: www.trainingforchange.org/

Shirika la Mabadiliko: www.thechangeagency.org/

Tamthiliya ya Kimataifa ya Asasi ya wanaonyanyaswa (wanatumia tamthiliya kama nyenzo ya mabadiliko ya kijamii): www.theatreoftheoppressed.org/en/index. php?nodeID=1

Sanduku la zana la jamii: mawazo, mbinu na zana kwa ajili ya upimaji shirikishi, ufuatiliaji na tathmini katika misitu ya jamii, Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa: www.fao.org/docrep/x5307e/x5307e00.HTM#Contents

Njia 100 za kuchangamsha vikundi: Michezo ya kutumia kwenye warsha, mikutano na kwenye jamii, Ushirikiano wa Kimataifa wa VVU/UKIMWI: www.icaso.org/vaccines_toolkit/subpages/files/ English/energiser_guide_eng.pdf

Vidokezo vya uwekezaji, michezo, na vichangamshi: warsha.350.org/facilitation/

Wanawake wa Umoja wa Mataifa, Jamii ya Vitendo, Mafunzo ya Jinsia: gtcop.unwomen.org/index. php?lang=en

# KIAMBATISHO A: MANENO YA JINSIA NA UFAFANUZI

## KANUNI ZA KIUTAMADUNI

Mawazo kwamba viwango vya maadili vinaweza kutofautiana kutoka sehemu moja hadi nyingine kulingana na kile jamii fulani au utamaduni unaamini kuwa ni kizuri au kibaya, sahihi au sio sahihi. Hili linaweza kusababisha imani kwamba maadili ya "kiutamaduni" yana kipaumbele yanapotofautiana na viwango vya haki za binadamu vinavyokubalika.

## UWEZO WA KUTAMBUA UTAMADUNI

Mtazamo ambao unatambua kwamba mabadiliko yanapaswa kujengwa, au hata kufikiria na kujibu, desturi za utamaduni zilizopo na ambao mradi unakusudia kuwanufaisha. Hii pia inatambua kwamba utamaduni ni wa aina mbalimbali na kwamba utamaduni unatofautiana.

## JINSIA

Wajibu na majukumu tofauti yanayofanywa na wanawake na wanaume. Haya yanafundishwa mapema mwanzo wa maisha na wakati wote wa maisha, kutoka kwa wale wanaotuzunguka — sio "asilia". Yanatofautiana kati ya utamaduni na maeneo, na hubadilika kadri muda unavyokwenda.

## KUTOTAMBUA JINSIA

Kushindwa kuzingatia tofauti kati ya mahitaji ya wanawake na wanaume, manufaa, na upataji wa rasilimali, madaraka na hadhi kijamii.

## UBAGUZI WA KIJINSIA

Ushughulikiaji wa watu kwa utaratibu, bila ya upendeleo kwa kuangalia jinsia yao, ambayo inawanyima haki, fursa au rasilimali.

## USAWA WA KIJINSIA

Haki sawa, hadhi, fursa na matokeo kwa wanawake na wanaume.

## HAKI YA KIJINSIA

Inawapa wanaume na wanawake haki sawa na stahiki katika vipengele vyote vya maendeleo ya binadamu. Hii inajumuisha haki za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kiraia na kisiasa; heshima sawa; na fursa sawa ya kufanya uchaguzi. Kupata haki sawa kwa wanawake na wanaume kunaweza kumaanisha kwamba wanapata huduma tofauti, kwa sababu mazingira yao ni tofauti.

## KUJALI JINSIA

Wakati mtu au programu inaweka nadharia ya "kujali jinsia" katika vitendo. Vitendo na mazoezi vinatumika kushughulikia masuala na matatizo kuhusiana na upendeleo na ubaguzi.

## KUTAMBUA UNYETI WA JINSIA

Kuonyesha kuelewa na kujali masuala ya utamaduni wa jamii unaohusiana na kujumuika pamoja kwa wanawake na wanaume katika mienendo kadhaa au fursa; uhusiano wa madaraka kati ya wanawake na wanaume; ubaguzi wa kijinsia; na mahitaji yao tofauti, matatizo na upataji wa rasilimali.

## MAGEUZI YA JINSIA

Pale ambapo jinsia inachukuliwa kama kiini cha kuendeleza usawa na kufanikisha matokeo mazuri ya maendeleo. Yanafanya kazi ya kubadilisha uhusiano wa jinsia usio sawa ili kuongeza kushirikiana madaraka, udhibiti wa rasilimali, kufanya uamuzi, na kusaidia uwezeshaji wanawake.

## HAKI ZA BINADAMU

Jambo fulani ambapo mtu ana madai sahihi, ambapo nchi na wengine wana wajibu na wanaweza kuwajibishwa. Inaweza kuwekwa katika sheria, kufafanuliwa na mila, na/au kama utaratibu wa jamii. Azimio la Dunia la 1948 la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu ni makubaliano ya kimataifa kuhusu haki za binadamu za watu wote, wakiwemo wanawake wote.

## KUWEZESHA WANAWAKE

Mchakato wa "kutoka chini-juu" wa kubadilisha uhusiano wa madaraka kati ya wanawake na wanaume. Inafanikishwa na mtu binafsi au vikundi vya watu, hususan wanawake, kutambua hadhi na madaraka ya chini ya wanawake, na kujenga uwezo wao wa kupinga na kubadilisha hilo. (mara nyingi neno hili linatumika katika namna rahisi, na sio wakati wote linaeleweka kama "kutoka chini-juu.


## HAKI ZA WANAWAKE

Azimio la 1948 la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu linaeleza haki za binadamu kwa wanawake na wanaume wote. Hata hivyo, maslahi ya kiutamaduni, kimaoni, kijamii, kiuchumi na kisiasa vimeunganishwa kuwatenga wanawake katika haki zao nyingi. Hivyo, haki za binadamu za wanawake zinahitaji kuzingatiwa kwa upekee na kupewa uzingativu maalumu.

Maneno na ufafanuzi huu ulifanyiwa majumuisho na Di Kilsby kwa ajili ya Oxfam Australia kama sehemu ya mradi ili kuboresha utaratibu wetu wenyewe wa jinsia.

# KIAMBATISHO B: PICHA ZA MALIASILI KWA AJILI YA ZOEZI LA 4

Mto, msitu, mlima, shamba, bahari.











# KIAMBATISHO C: MAONYESHO YA JUKWAANI

## UTANGULIZI WA MAONYESHO YA JUKWAANI

*"Mchezo wa kuigiza ni aina ya maarifa: Inapaswa na pia inaweza kuwa njia ya kuibadilisha jamii. Mchezo wa kuigiza unaweza kutusaidia kuimarisha siku zetu zijazo, badala ya kuisubiria." (Augusto Boal)*

Kabla ya kuanza kufanya mazoezi ya Maonyesho ya Jukwaani, ni muhimu kwamba mfundishaji awe na uelewa wa baadhi ya dhana za msingi na vipengele vya nadharia na maonyesho ya jukwaani

Maonyesho ya jukwaani yalianzishwa na muigizaji wa Brazili Augusto Boal katika miaka ya 1970. Maonyesho ya jukwaani ni mchezo wa kuigiza kwa ajili ya kila mtu. Ni mchezo wa kuigiza ambao uko kinyume na jamii. Maonyesho ya jukwaani yanakusudia kutoa demokrasia ya watu kupata sanaa na utamaduni, sio tu kama watumiaji wasiokuwa watendaji, lakini kama washiriki hai na watendaji katika mchakato wa kugundua upya rasilimali zao za ubunifu.

Maonyesho ya jukwaani ni aina ya mchezo wa kuigiza wa jamii ambao ni wa kuwasiliana na shirikishi. Katika mchezo huo mgogoro wa jamii au suala la ugomvi linaigizwa, pamoja na watazamaji (wanaofahamika kama "waigizaji watazamaji" "spect-actors") wanahamasishwa kuingia katika utendaji, kumbadili mmoja kati ya wahusika na kujaribu kubadilisha vizuri matokeo jukwaani. Watazamaji kisha wanachukua kile walichojifunza na kukitumia katika maisha yao halisi. Maonyesho ya jukwaani ni majaribio ya vitendo vya maisha ya siku zijazo. Ni fursa pekee ya kubainisha na kujaribisha mikakati ya mabadiliko katika eneo salama la mchezo wa kuigiza.

### Mandhari ya jukwaa, sauti, Namna ya kuigiza na vifaa

Uigizaji wa maonyesho ya jukwaani unaweza kufanyika mahali popote. Hakuna kitu cha kisasa sana kinahitajika lakini kama muda na vifaa vinaruhusu, mchezo unapaswa kufanywa mahali panapoonekana. Kama ikiwezekana, vitu vinavyoonekana katika jamii vinapaswa kutumika. Mavazi ya uigizaji yanaweza kutumika na yanapaswa kufanya hali ya muigizaji kuwa dhahiri.

Waigizaji wanapaswa kuhamasishwa kuzungumza kwa sauti na kuwatazama watazamaji wakati wanazungumza. Njia nyingine za kusikika na kuona (nyimbo, mashairi, n.k.) zinapaswa kujumuishwa ili kuufanya mchezo uwe dhahiri zaidi.

### Wahusika/ Wajibu wa mwigizaji katika Maonyesho ya Jukwaani

Wakati wa kupanga hatua ya programu ya mafunzo ya Ridhaa inayotolewa kwa Uhuru, Kabla na Baada ya kupata Taarifa za Kutosha, mfundishaji anatakiwa kuamua iwapo:

- wacheze wahusika peke yao
- awaalike baadhi ya washiriki wa mafunzo kuchukua nafasi za wahusika katika mchezo
- aalike kundi la waigizaji kutoka nje (au watu ambao wanajisikia vizuri au wako tayari kuigiza) ili kuigiza mchezo huo.
- Katika namna yoyote, waigizaj iwanahitaji kupewa muda wa kujikumbusha mswada na kujifunza kuhusu mambo muhimu (k.v, utembeaji wao jukwaani wakati wa mchezo).

Kwa ujumla:

- Wahusika katika mchezo wanapaswa kukaribia maisha halisi au kuigiza maisha halisi na sio kama picha ya vichekesho inayoonyesha mtindo usisobadilika wa watu. Wanapaswa kushirikishana mila, desturi na maadili yanayofanana na watazamaji kama vile lugha/lahaja, majina, shughuli, taratibu za kila siku na kila wiki, chakula, ladha n.k.
- Ni muhimu sana kwamba waigizaji wawaelewe wahusika wanaocheza nafasi zao. Wanapaswa kuelewa vya kutosha kuhusu mada na wahusika wake ili kufanya kwa haraka wakati wa maonyesho.

- Waigizaji lazima wasikilize kwa makini uingiliaji wa waigizaji watazamaji'
- Waigizaji lazima wawe na uwezo wa kufanya kwa haraka papo hapo na kujibu kwa watazamaji mawazo katika njia ambayo inafanana na wahusika wao.
- Waigizaji hawatakiwi kukataa tu (au kufuata kwa furaha) wazo la mwigizaji mtazamaji bali wanapaswa kufuata mbinu ya "Ndiyo, lakini", kumkosoa mwigizaji mtazamaji kushiriki kwa undani matatizo mchezoni.

## Mwigizaji mtazamaji

Mwigizaji mtazamaji ni mtazamaji ambaye anaingia jukwaani na kuchukua nafasi katika mchezo ("Uingiliaji"). Waigizaji watazamaji huangalia njia mbadala kwa ajili ya mhusika mkuu (na katika baadhi ya mazingira mhusika mpinzani) kubadilisha matokeo ya mchezo. Mwigizaji mkuu ni mhusika mkuu au jasiri katika mchezo wakati mwigizaji mpinzani ni mshindani ( sio wakati wote awe adui) anayemzuia mhusika mkuu kupata kile anachokitaka. Katika Maonysho ya jukwaani, mwigizaji mpinzani mara nyingi hushindwa kufanikisha lengo lake na watazamaji huombwa kumbadili na kujaribisha mawazo yake kwa ajili ya mabadiliko.

## Mfanya mzaha

Mfanya mzaha ndiye mmiliki mwigizaji wa Maonyesho ya Jukwaani — huyu atakuwa mmoja kati ya wafundishaji wa FPIC. Anafafanua matokeo kwa ajili ya watazamaji, anawezesha uingiliaji wa watazamaji, na kusaidia kuakisi uingiliaji pamoja na watazamaji. Sehemu hii ya pili ni muhimu na inahusisha kukosoa watazamaji kujihusisha kwa kina katika masuala yaliyopo. Hata hivyo, kukosoa watazamaji haimaanishi kuanzisha wazo la mtu. Kinyume chake, kazi kubwa ya mfanya mzaha ni kuuliza maswali ambayo yatasidia kuimarisha uelewa (ikiwa ni pamoja na wa mfanyamzaha) wa jambo hilo.

Hakuna mtindo mmoja wa "Ufanyaji mzaha" katika Mchezo wa Maonyesho ya Jukwaani. Wafanya mizaha huonyesha hadhi yao na njia za kujihusisha na watazamaji. Hata hivyo, mfanya mzaha:

- ni mwenye nguvu na mwenye shauku kuhusu mchakato huo
- ni msikilizaji mzuri
- hatoi hukumu
- anajiamini katika wajibu kama kiongozi, na sio kama mtu anayefahamu majibu ya mambo yote yanayojitokeza
- anafahamu mwenendo ndani ya chumba
- anakubali mabadiliko ya mipango yake
- huimarisha majadiliano na kufanya tukio lisonge mbele
- anaepuka vitendo vyote ambavyo vinaweza kuwachezea au kuwahamasisha watazamaji
- anajua kwamba jinsi anavyotoa majibu mengi, ndivyo kunavyokuwa na nafasi chache kwa ajili ya ushiriki wa watazamaji
- huuliza maswali ya wazi, kuepuka maswali yenye majibu ya "ndiyo" na "hapana"
- anauliza kila swali kwa uhakika akisubiri kusikia jibu
- anaelewa kwamba watu wanahitaji muda wa kufikiria mambo
- anaepuka mjadala mrefu na watazamaji na anawahamasisha watazamaji kujaribu utatuzi wao jukwaani
- anafahamu kwamba wakati wote kutakuwa na masuluhisho zaidi ya moja kwa tatizo lolote
- lazima atafute masuluhisho ya kiajabu na kuwataka watazamaji waamue
- huhakikisha mtu aliyeingilia kati hatoki jukwaani akiwa ameshindwa.

## Kufanyia mzaha tukio katika Maonyesho ya Jukwaani

Kila tukio la Maonyesho ya Jukwaani hujumuisha maonyesho mawili: Uwasiishaji wa kile kinachoitwa "si mfano wa kuigwa" (hili ni onyesho linalofanywa na waigizaji kwa kuzingatia mswada wanaogiza) kwa ajili ya watazamaji kujua mchezo unahusu nini; na kisha Onyesho halisi ambalo watazamaji wanaalikwa kuja jukwaani na kujaribu mawazo yao kwa ajili ya mabadiliko.

Kwa upande wa muda wa kuigiza tukio la Maonyesho ya Jukwaani, hili hutegemeana na urefu, pamoja na majibu ya watazamaji katika mchezo. Kwa ujumla, tukio katika Maonyesho ya Jukwaani hufanyika kati ya dakika 60–90.

Uchekeshaji unaweza kugawanyika katika awamu nne:

## Awamu ya 1: Kabla ya onyesho la mfano usio wa kuigwa

Wakati wa awamu hii, mfanya mzaha, kwa kawaida husimama katikati ya jukwaa, huwakaribisha watazamaji, hujitambulisha, (na wakati mwingine kutambulisha waigizaji), anafafanua aina ya mchezo na kuelezea tofauti za msingi kati ya aina ya mchezo wa kuigiza usiokuwa shirikishi na maonyesho ya jukwaani kama shirikishi, mchezo unaosukumwa na watazamaji. Ni muhimu kufuata uanzishaji wa Maonyesho ya jukwaani kwa kila watazamaji tofauti. Wanafahamu kiasi gani kuusu Maonyesho ya Jukwaani? Utauwezeshaje utangulizi ili ulete maana kwa watazamaji?

Katika baadhi ya mazingira, inaweza kufaa kuwawezesha watazamaji kufahamu kwamba hakuna waigizaji wanaoocheza peke yao. Mwisho, mfanya mzaha hukabidhi mchezo kwa waigizaji na mchezo kuanza.

*"Ufuatao ni mchezo!"*

## Awamu ya 2: Wakati wa uigizaji wa mfano usiofaa kuigwa na mwanzo wa maonyesho ya jukwaani

Baada ya mchezo kuisha, mfanya mzaha hurejea jukwaani na kuwashirikisha watazamaji katika mahojiano mafupi kuhusu mchezo. Anaweza kuuliza maswali kama:

- Nini kilitokea wakati wa mchezo?
- Ni masuala na matatizo gani uliyoyaona?
- Nani ni wahusika wakuu?
- Je, mhusika mkuu anataka nini?
- Je, mhusika mkuu alipata alichokuwa anakitaka?
- Nini kilimzuia kupata alichokuwa anakitaka?
- Ni kitu gani kingine angekifanyaili kupata alichokitaka katika hali hii?
- Je, matatizo haya yapo katika jamii yetu?

Lengo ni kuwashirikisha watazamaji wengi iwezekanavyo, kuwafanya washirikishane mawazo yao na kuwachangamsha katika wazo la kushiriki katika tukio la Maonyesho ya Jukwaani Kisha, Mfanya mzaha anafafanua sheria za Mchezo wa Maonyesho ya Jukwaani:

"Tafadhali piga kelele 'Acha' unapokuwa na wazo la kile ambacho mhusika mkuu anaweza kufanya kutoa athari chanya za matokeo ya mchezo. Njoo jukwaani; chukua jukumu la mhusika unayetaka kumbadili na jaribu wazo lako."

Mfanya mzaha anaweza kutaka kucheza mchezo wa "pasha" (kwa mfano, alama mkasi na Zungushia — tazama hapo chini) kuwaandaa watazamaji kuja jukwaani na kuingilia mchezo.

*"Ufuatao ni mchezo tena!"*

## Awamu ya 3: Wakati wa Maonyesho ya Jukwaani

Wakati wa Maonyesho, mfanya mzaha anapaswa kuwa mahali katika upande wa jukwaa, akiwatazama watazamaji (sio waigizaji) ili kuwabainisha watazamaji kwa haraka ambao wako tayari kuingilia kati mchezo. Mara watazamaji (mwigizaji mkuu) anapofika jukwaani, mfanya mzaha anaweza kuuliza:

- Jina lako ni nani?
- Ungependa kumbadili nani?
- Ungependa kuingilia kati kuanzia katika tukio gani la mchezo?

Wakati wa kuingilia kati mfanya mzaha anapaswa kuzingatia kwa karibu kile ambacho watazamaji wanajaribu kufanya, vyote kwa maneno yake pamoja na vitendo na ishara. Wakati uingiliaji unapofikia mwisho, mfanya mzaha

kwanza anawaalika watazamaji wengine kujadili uingiliaji kati:

- Umeshuhudia nini wakati wa uingiliaji kati?
- Je, mtu huyu alianya nini tofauti na mtu wa awali?
- Je, alipata kile alichokitaka?
- Je, ilikuwa na uhalisia? Je, hili lilitokea kabla
- Je, uchaguzi huo ulifaa kwa kila mmoja?
- Je, ni vitu gani vingine anavyoweza kufanya katika hali hii?

Wakati huo, mfanya mzaha anaweza pia kushirikisha waigizaji na kuwauliza maswali kuhusu uingiliaji kati kwa mtazamo wa wahusika wao. Mwisho, Mfanya mzaha anaweza kuuliza kama mtazamaji mwingine ana mawazo tofauti ya namna ya kushughulikia tatizo wakati huohuo. Kama hakuna yeyote mwenye wazo jingine wakati huu, mchezo uendelea (kuanzia katika tukio linalofuata) kama vile hakuna kilichotokea hadi mwigizaji mtazamaji atakapopata fursa ya kuja na kujaribu wazo lake.

## Awamu ya 4: Baada ya Maonyesho ya Jukwaani

Tukio la Mchezo wa maonyesho ya jukwaani unamalizika kwa Mfanya mzaha kuwashukuru watazamaji kwa ushiriki wao na waigizaji kwa kazi yao. Mfanya mzaha pia anawaalika watazamaji kuchukua kile walichojifunza wakati wa tukio na kukitumia katika maisha yao halisi.

## Mchezo wa hiari wa pasha kabla ya kuanza kwa Maonyesho ya jukwaani

**Alama ya Mkasi na Duara**

Malengo:
Kupasha kwa ajili ya watazamaji wa Mchezo wa Maonyesho ya jukwaani

Idadi ya watu:
Kila mmoja; washiriki wa programu ya mafunzo, waigizaji na Mfanya mzaha

Muda:
Dakika 5

Mchakato:

- Mfanya mzaha anawataka washiriki kufanya duara kwa kutumia mikono yao ya kulia.
- Kisha wanapaswa kufanya alama ya mkasi kwa kutumia mikono yao ya kulia.
- Mwisho, wanapaswa kufanya yote kwa wakati mmoja

## Michezo mingine ya kuigiza inayoweza kufanyika kabla ya kuanza kwa tukio la Mchezo wa Maonyesho ya jukwaani

**Duara Kistari**

Malengo:
Kupasha, uimarishaji wa kundi

Idadi ya watu:
Kila mmoja; washiriki wa programu ya mafunzo, waigizaji na Mfanya mzaha

Muda:
Dakika 10–15

Mchakato:

- Huu ni mchezo wa kimya.
- Kundi linatengeneza duara pamoja na mtu mmoja anayejitolea kuingia katikati.
- Mfanya mzaha anafafanua kwamba lengo la mchezo ni kwa watu wawili wowote katika duara kuonyesha ishara kimyakimya na kwa haraka kubadilishana nafasi.
- Mtu aliyepo katikati anajaribu kuingia katika nafasi mojawapo iliyowazi kabla washiriki hawajabadilishana vizuri nafasi. Mtu anayeachwa anachukua nafasi katikati.
- Mwishoni mwa zoezi, Mfanya mzaha anaweza kuwauliza washiriki walijisikiaje kuhusu zoe.

**Matembezi ya Hisani**

Malengo:
Kujenga uaminifu, kufanya kazi kwa pamoja, kuhisi kile tunachokigusa

Idadi ya watu:

Kila mmoja; washiriki wa programu ya mafunzo, waigizaji na mfanya mzaha

Muda:

Dakika 10–15

Mchakato:

- Washiriki wagawanyike katika makundi. Mtu A ni muongozaji na anamuongoza Mtu B, akiwa amefumba macho yake, kuzunguka chumba. Kila mmoja kwa kipindi fulani, A atamtaka B aguse kitu kilichomo chumbani. B atatumia muda kukihisi kitu hicho.
- Baada ya muda, watu wabadilishane wajibu.
- Hili ni zoezi la kimya.
- Mwishoni mwa zoezi, Mfanya mzaha anaweza kuwauliza washiriki walivyojisikia kuhusiana na zoezi na namna mchezo ulivyohusianishwa na mada kuu ya tukio la Mchezo wa Maonyesho ya jukwaani.
- Kabla yakujadili zoezi hili katika kundi zima, kila watu wawiliwawili watakuwa wamepewa dakika ya kujadili uzoefu wao.

## MSWADA WA MCHEZO WA MONYESHO YA JUKWAANI KWA AJILI YA ZOEZI LA 5

Ni muhimu kusisitiza tena kwamba katika Mchezo wa Maonyesho ya Jukwaani wakati wote tunaionyesha dunia kama ilivyo; yaani wakati wa mchezo halisi tunatangaza tatizo na madhara yake lakini kamwe tunachokifikiria ni suluhisho. Katika maneno mengine, tunawaonyesha watazamaji "mfano usio wa kuigwa" na kisha kuwaalika kuja jukwaani na kujaribu mawazo yao kwa ajili ya mabadiliko mazuri, ambayo baadaye hujadiliwa na watazamaji, ambayo yanaruhusu mazungumzo ya kina yanayoongozwa na jamii kuhusu masuala nyeti na migogoro.

Hapa, mswada ufuatao unaonyesha mfano wa jinsi ridhaa ya jamii inavyoweza kutolewa pasipo uhuru.

Mswada unawasilishwa kama "nakshi" badala ya kuwa rasmi, mswada wa njia ya mazungumzo. Hii inaruhusu uhuru mkubwa kwa wafundishaji wa FPIC kutumia mazungumzo halisi katika mahitaji yao na maudhui.

Muda wa onyesho halisi haupaswi kuzidi dakika 10–12, hivyo muda huo muhimu umetolewa kwa uingiliaji kati wa Monyeshoya jukwaani na majadiliano.

Kabla ya kuanza mchezo, mfanya mzaha anapaswa kuanza Awamu ya 1 ya mchakato wa uwezeshaji.

### Onyesho la 1

Mwanzishaji wa mradi anatembelea jamii ya wenyeji na kukutana na kundi la wawakilishi wa jamii. Amevaa mavazi rasmi, anazungumza kidogo au hazungumzi lugha ya wenyeji, na kuanzia mwanzo, anasisitiza uhitaji wa hatua za haraka kuhusiana na masuala muhimu aliyokuja kujadiliana na jamii katika hali ya kuheshimiana, kuaminiana na ushirikiano, ambayo atahakikisha kwamba kila mmoja atafaidi kutokana na jitihada zilizopendekezwa.

Wawakilishi wa wenyeji wanamshukuru kwa upole mwanzishaji wa mradi kwa kuwatembelea na kupendekeza kupata chakula pamoja kabla ya kuzungumzia biashara, lakini kwa mara nyingine tena mwanzishaji wa mradi anabainisha uhitaji wa maamuzi ya haraka, anakataa mapumziko yoyote yasiyokuwa ya muhimu na kuendelea kufafanua faida kubwa za jitihada ambazo yupo kwa ajili ya kuziendeleza. Anafungua kompyuta yake ndogo inayong'aa na kuanza uwasilishaji wake wa kutumia vyombo vya kisasa kwa njia ya PowerPoint, wote kwa Kiingereza, pamoja na chati na takwimu zinazoonekana kuwa ngumu. Anarudia kusisitiza hali ya kisayansi ya data zote; akitoa mifano ya matukio yaliyofanikiwa kutoka katika maeneo mengine ya dunia; anatolea mifano ya faida nyingi kwa jamii katika maendeleo ya kiuchumi na, hususani, uongezaji wa ajira, na kuhitimisha kwa kusema kwamba huu ni mradi mkubwa usiokuwa na hatari ndiyo pekee unaopatikana kwa jamii kuwa sehemu ya kile kilichokuwa nguvu zisizozuilika kwa mambo mazuri duniani yaani utandawazi.

Wakati wawakilishi wa jamii wanapojaribu kuuliza maswali kuhusiana na aina ya mradi, mwanzishaji wa mradi anajibu kwa kuwapa nyaraka kubwa ili wazisome na kufanya uamuzi wenye taarifa za kutosha. Anawapa pia nakala ya mkataba. Mwanzishaji wa mradi anaanza kukusanya na kufungasha vitu vyake na kuwaagiza wawakilishi wa jamii kumtembelea mjini wiki moja kuanzia sasa. Wawakilishi wa jamii wanaomba muda zaidi kuweza kushauriana na jamii yao lakini mwanzishaji wa mradi anasisitiza kwamba uamuzi wa mwisho unatakiwa kufanyika haraka iwezekanavyo kwa kuwa muda ni mali na katika wakati huu wa mgogoro wa kiuchumi maisha yanawaadhibu wale wote wanaochelewa.

*Je, unataka kuwajibika kwa kuanguka zaidi kwa jamii yako nzuri? Tutakutana wiki lijalo. Usichelewe. Kuna jamii nyingine zenye shauku sawa ya kutia saini.*

### Onyesho la 2

Wawakilishi wa jamii wamebaki peke yao na wanapitia nyaraka. Wanakutana na changamoto kubwa ya lugha ya kiufundi, isiyoeleweka na dhana zote zimeandikwa kwa Kiingereza, lugha ambayo hakuna hata mmoja wao anayeijua vizuri. Wanachokielewa ni kutokana na brosha, hata hivyo, ni kwamba mradi huu utakuwa na thamani kubwa ya kuichumi kwa jamii yao pamoja na madhara machache sana ya mazingira, vyotehivyo vitazuiliwa na kampuni bila kuwa na wajibu mwingine wa nyongeza wala gharama kwa jamii. Wawakilishi wa jamii wanajadiliana kwa hisia faida na hasara za mradi huo na wamepewa muda wa wiki moja tu, kuamua bila kushauriana na wanajamii wengine katika hatua hii pamoja na kikwazo cha mmoja kati ya wawakilishi hao. Kisha wanaamua kwenda mjini na kuhakikisha kuwa maswali yao yatasikilizwa watakapokuwa wakirudia kukiri uhitaji wa muhimu kwa uendelezaji wa jamii yao,

au vinginevyo hivi karibuni vijana wao watahamia katika mji mkubwa unaofuata, ambapo hali ya jamii itazidi kuwa mbaya.

*Hakuna uchaguzi mwingine. Tunautaka mradi huu. Uamuzi wetu uko wazi. Lakini tunatakiwa kuhakikisha kwamba jamii yetu itafaidika kutokana na mradi huu.*

### Onyesho la 3

Wiki moja baadaye, wawakilishi wa jamii wanawasili katika ofisi za mwanzishaji wa mradi zilizopo katika wilaya ya biashara za kifahari katika mji mkuu. Ilikuwa vigumu kwao kufika hapo kwani wametakiwa kutumia gharama kubwa ya usafiri na wanaweza kutumia usafiri wa kawaida. Wamechoka na miili yao inauma. Ofisi imejaa samani za kifahari na hali ya hewa ni rasmi na hawajaizoea. Bado wawakilishi wa jamii wanajisikia kama wamekuja wakiwa wamejiandaa vizuri na wako tayari kujadiliana mkataba ambao kwa kweli utaisaidia jamii yao ambayo haina maendeleo.

Wanapoendelea kukaa na kusubiri miadi yao, wawakilishi wa jamii wanashuhudia mwanaume akiondoka katika ofisi ya mwanzishaji mradi akionekana kuwa na masikitiko. Anapitisha macho kwa haraka kwa wawakilishi wa jamii kabla ya kuongea kwa sauti kuelezea kuchanganyikiwa kwake kutokana na kudanganywa na mwanzishaji wa mradi.

Wawakilishi wa jamii wanatazamana kwa wasiwasi na wakati wanamkaribia mtu huyo mwanzishaji wa mradi anatoka nje na kuwakaribisha akiwa na uchangamfu mkubwa. Anawakaribisha haraka ofisini kwake, anawaagiza kukaa chini na baada ya kuwajulia hali zao na kuwapatia glasi za maji ya kunywa, anaanza moja kwa moja kuzungumzia kuhusu biashara kwa kupaza sauti yake kwa uamuzi mkubwa na kuridhika ambako leo itakuwa ni siku ambayo hakuna hata mmoja wao atakayeisahau muda wowote hivi karibuni.

Kikao kinaanza kwa mwanzishaji wa mradi kuthibitisha tena umuhimu wa kufanya maamuzi kwa haraka. Anakaribisha dakika tano za maswali kuhusiana na mradi. Wawakilishi wanauliza kuhusu hatari ya usalama, namna faida za kiuchumi zitakavyogawanywa na kuomba muda zaidi wa kushauriana zaidi na jamii. Kwa kujibu, mwanzishaji wa mradi anaonyesha dalilii za kutetemeka, na kuongeza sauti yake akirudia kusema mradi hauna hatari yoyote, akiweka wazi kwamba uamuzi unatakiwa kufanyika haraka na kuhitimisha kwa kusema kwamba hii ni fursa ya sasa la sivyo haitatokea tena. Akirejea katika hali yake ya awali ya kirafiki, huku akitabasamu anawaagiza wawakilishi wa jamii kutosimamia zaidi katika maendeleo ya kiuchumi yanayohitajika na maendeleo, hususan kwa vijana wa jamii hiyo. Alieleza pia ukweli kwamba katika siku za hivi karibuni watu wanaopinga jitihada za uchumi wa kiwango cha juu wamekuwa wakishambuliwa na wanajamii wenzao, jambo ambalo halipaswi kurudiwa siku zijazo kwani umwagaji wa damu ni mbaya kwa biashara. Anaweka mkataba mbele yao. Wawakilishi wa jamii wanaangaliana wakigundua kuwa sio rahisi, kisha wanakubali kwa kutikisa vichwa na kusaini mkataba.

*Hongereni. Mmeiokoa jamii yenu dhidi ya kifo.*

Mwisho

Katika hatua hii, mfanya mzaha anarejea jukwaani na kuanza uwezeshaji wa Awamu ya 2 hadi ya 4.

## MSWADA WA MCHEZO WA MAONYESHO YA JUKWAANI KWA AJILI YA ZOEZI LA 13

Mswada ufuatao unaonyesha mfano wa jinsi wanajamii wasivyokuwa na uwezo wa kujadiliana kwa haki pamoja na mwanzishaji wa mradi.

### Onyesho la 1

Jamii ya wenyeji inakutana kwa pamoja kujadili umuhimu wa mkutano ujao pamoja na mwanzishaji wa mradi ambaye anaahidi faida zitakazoletwa kwa ajili ya jamii lakini pia anatoa idadi kubwa ya madhara yanayohitaji kuchunguzwa ili kuhakikisha kwamba makubaliano yanayofanyika yataongeza kwa kiasi kikubwa maendeleo ya kiuchumi kwa watu wa jamii waliokuwa wakipata shida kwa muda mrefu.

Muda mfupi baada ya kuanza rasmi, wanawake wengi katika kundi wanaagizwa kuondoka mahali pale ili wakalete chakula na vinywaji ambavyo vitagaiwiwa wakati wa kuhitimisha mkutano. Wakati mwanamke mmojawapo anapoongea kwa sauti ya upole kuonyesha umuhimu wa wanawake katika jamii kuwa na wajibu hai katika majadiliano, mzee mmoja wa jamii anamhakikishia kwamba mahitaji wa wanawake yana umuhimu mkubwa zaidi na yatazingatiwa.

Wanawake wanaondoka. Mkutano unaendelea na kwa muda mfupi, mwanajamii tofauti anauliza maswali muhimu.

*Je, ni faida gani hasa ambazo jamii itapata? Je, ni madhara gani hasa yanayoweza kutokea kutokana na jitihada zinazopendekezwa? Je, faida hizo zitagawanywaje?*

Hata hivyo, kutokana na ugumu na muda wa majadiliano yanayotarajiwa, viongozi wawilii wa jamii, wote wanaume na wenye umri mkubwa, wanapewa kazi ya kuunda kamati ya wataalamu ambayo itachunguza taarifa zote za mkataba unaotarajiwa. Ingawa sio kila mmoja anakubaliana na uamuzi huo, wanajamii wengine kimsingi wanaondoka mkutanoni. Viongozi wanawahakikishia mahitaji yao yatazingatiwa kikamilifu.

*Wengine wanahakikishiwa kwamba njia zetu za utu na mila zetu za maisha hazipo kwa ajili ya kuuzwa na kwamba kila mmoja, na kwa hilo tunamaanisha kila mmoja, atafaidi kutokana na mkataba uliopendekezwa.*

## Onyesho la 2

Viongozi wawili wa jamii wanasafiri kwenda katika mji mkuu kukutana na mwanzishaji wa mradi, wakiongozana na katibu wake, ili kujadili mradi mkubwa wa maendeleo uliopendekezwa. Amevaa mavazi rasmi, anazungumza kidogo au hazungumzi lugha ya wenyeji, na kuanzia mwanzo, anasisitiza uhitaji wa hatua za haraka kuhusiana na masuala muhimu aliyokuja kujadiliana na jamii katika hali ya kuheshimiana, kuaminiana na ushirikiano, ambao utahakikisha kwamba kila mmoja atafaidi kutokana na jitihada zilizopendekezwa.

Mwanzishaji wa mradi anawasilisha chati na takwimu nyingi zinazoonekana kuwa ngumu. Anarudia kusisitiza hali ya kisayansi ya data zote; akitoa mifano ya matukio yaliyofanikiwa kutoka katika maeneo mengine ya dunia; anatolea mifano ya faida nyingi kwa jamii katika maendeleo ya kiuchumi na, hususani, uongezaji wa ajira, na kuhitimisha kwa kusema kwamba huu ni mradi mkubwa usiokuwa na hatari ndiyo pekee unaopatikana kwa jamii kuwa sehemu ya kile kilichokuwa nguvu zisizozuilika kwa mambo mazuri duniani yaani utandawazi. Wawakilishi wa jamii wamechoshwa na lugha ya kiufundi iliyotumiwa na mwanzishaji wa mradi. Wanachukua vijitabu vyao vya kuandikia kumbukumbu ili kuandika baadhi ya hoja muhimu zilizoorodheshwa lakini mwanzishaji wa mradi anawahakikishia kwamba hakuna uhitaji wa kuandika katika karatasi

*Karatasi nyingi zinamaanisha miti michache.*

Na anawaambia kwamba katibu wake anachukua kumbukumbu ambazo zitatumiwa na wao pia pale zitakapotakiwa. Kiongozi wa jamii anaacha kuchukua kumbukumbu na kuendelea kuuliza mfumo utakaotumika kwa ajili ya ugawanaji wa faida na kiasi gani ambacho mwekezaji atapata katika mradi huo. Mwanzishaji wa mradi, taratibu anaanza kukerwa akiwahakikishia kwamba hawatakiwi kuwa na wasiwasi na jamii itapata kitu kizuri katika kipindi hiki cha uchumi mgumu. Wawakilishi wa jamii wanakubali kwa kutikisa kichwa, wakionyesha shukurani zao kwa jitihada zilizopendekezwa na kuomba muda zaidi kwa ajili ya kushauriana na jamii yao nzima kwani hawawezi kukubaliana na mradi bila kuwa na mazungumzo zaidi na jamii. Aidha, wanapendekeza kufanya mazungumzo ya awamu nyingine katika jamii ili mwanzishaji wa mradi apate uelewa wa kina na wa binafsi, pamoja na wawakilishi wa jamii kuepuka kukabiliwa na shtuma za kuingia makubaliano bila kuwashirikisha wanajamii wengine.

Pendekezo limekataliwa kabisa na mwanzishaji wa mradi.

*Msinishirikishe katika matatizo yenu ya ndani.*

Anasisitiza kwamba uamuzi wa mwisho unapaswa kufanyika haraka iwezekanavyo kwa kuwa muda ni mali na katika kipindi cha mgogoro wa kiuchumo duniani, maisha yanawaadhibu wale wanaochelewa. Kisha anawaagiza viongozi wa jamii kusaini karatasi ambazo hazijaandikwa kitu ambazo baadaye atazijazia taarifa nyingine za makubaliano ya awali, ikiwa ni pamoja na vigezo na masharti ambayo yanayoshughulikia madhara ya mradi kiuchumi, kijamii na kimazingira na kupunguza madhara yanayoweza kutokea katika mradi.

Wakatii viongozi hao wawili wa jamii wanaposita kusaini, mwanzishaji wa mradi kwa uchangamfu anawahakikishia kwamba hawapaswi kuwa na wasiwasi wowote.

*Sasa ni wakati wa utekelezaji na kuhakikisha kupona kwa muda mrefu kwa jamii yenu nzuri. Niamini mimi, mara hii itakapokamilika na kufanyika, wote tutakuwa kitu kimoja, familia tajiri na zenye furaha.*

*Wakati akisema maneno haya, anawapa mkononi bahasha zenye fedha nyingi. Wawakilishi wa jamii wanatazamana kwa haraka, wanatabasamu kwa kuona haya, wanachukua bahasha na kusaini makubaliano ya awali.*

## Onyesho la 3

Wiki chache baadaye. Mwanzishaji wa mradi, akiandamana na mwanasheria na polisi mwenyeji, wanaitembelea jamii kuwasilisha waraka rasmi unaoeleza kwamba wananchi wanatakiwa kuhama ili kuacha eneo kwa ajili ya mradi wa maendeleo unaohitajika sana. Wanajamii, wanaongozwa na wawakilishi wawili, wanashitushwa na kukataa kusaini mkataba wowote rasmi. Hata hivyo, kwa mshangao wao mkubwa, mwanzishaji wa mradi anatoa karatasi iliyoandikwa "Makubaliano ya Maandishi", yaliyosainiwa kwa uwazi na wawakilishi wa jamii.

*Makubaliano ni makubaliano. Hivyo mnaweza kutuachia nafasi na kuacha kuzuia kazi zetu tafadhali. Hatuna muda wa kupoteza.*

Wanakijiji wamekasirishwa na wanawakabili wawakilishi wa jamii. Wawakilishi wa jamii wanasisitiza kwamba hawana hatia na wanapendekeza kutoukubali mkataba. Wanamwendea mwanzishaji wa mradi na wasaidizi wake na kuwafahamisha kuhusu uamuzi wao wa kutohama. Mwanasheria anarudia kusema kwamba kuna mkataba wa maandishi ambao hauwezi kuvunjwa na kuvunjwa kwa mkataba huo kutasababisha kuwaondoa kwa nguvu. Wanakijiji wanajaribu kufikiria kwa pamoja nao.

*Tumeishi hapa kwa vizazi vingi. Hii ni ardhi ya babu zetu.*

Lakini bila mafanikio. Polisi anawaamuru wanakijiji kuhama haraka katika nyumba zao. Wanapokataa kufanya hivyo na kutangaza mgomo usiokuwa na vurugu, mwanzishaji wa mradi anakosa uvumilivu na kuagiza polisi kuacha kufanya michezo na afanye kazi yake. Polisi anatoa kirungu chake na kuanza kuwapiga watu. Mwanzishaji wa mradi anaangalia kinachofanyika na kutabasamu.

*Niachieni hakuna uamuzi mwingine. Ambaye hatasikia atahisi. Hakuna uamuzi mwingine. Kinachotakiwa kufanyika lazima kifanyike.*

Mwisho

Katika hatua hii, mfanya mzaha anarejea jukwaani na kuanza uwezeshaji wa Awamu ya 2 hadi ya 4.

# KIAMBATISHO D: MATUKIO YA ZOEZI LA 6

## TUKIO LA 1

Umeliona tangazo katika gazeti la taifa linaloelezea kwamba serikali inashughulikia maombi ya kampuni ya mafuta ya nazi kwa ajili ya kufungua shamba kubwa karibu na jamii yenu. Katika tangazo hilo, serikali imeeleza kwamba itashauriana na jamii zitakazoathirika kwa miezi 12 ijayo kuelewa maoni ya jamii kabla haijafanya uamuzi kuhusu mradi huo. Serikali itaitisha mkutano wa jamii mwezi ujao kuanza mchakato wa mashauriano.

1. Je, tukio hili linafafanua unachokifikiria kuwa ni ridhaa inayotolewa "kabla"?
2. Je, ni hatua gani ambazo jamii hii inatakiwa kuchukua kuhusiana na tukio hili?
3. Kama jamii imekuwa katika hali hii kabla walifanya nini? Matokeo yake yalikuwa nini?

## TUKIO LA 2

Umeona watu wa serikali na wa kampuni ya uchimbaji madini katika mji wako. Jirani yako ameona vifaa vya kuchimbia, vifaa vya kufanya upimaji na magari makubwa katika barabara za karibu. Huna uhakika wa nini ambacho watu wa serikali na wachimbaji madini wanakifanya katika jamii yako lakini wanaonekana kufanya kitu fulani. Wewe na jirani yako mnaamua kutafuta ukweli. Mnagundua kwamba kampuni ina kibali cha uchimbaji madini. Una wasiwasi kwamba machimbo katika jamii yako yatakuwa na madhara mabaya kwa mito ya eneo hilo na utafutaji wenu wa riziki.

1. Je, tukio hili linafafanua unachokifikiria kuwa ni ridhaa inayotolewa "kabla"?
2. Je, ni hatua gani ambazo jamii hii inatakiwa kuchukua kuhusiana na tukio hili?
3. Kama jamii imekuwa katika hali hii kabla walifanya nini? Matokeo yake yalikuwa nini?

## TUKIO LA 3

Unaamka asubuhi moja na kusikia sauti ya misumeno. Wewe, familia yako na majirani zenu mnatoka kijijini kwenu na kwenda zinakosikika sauti. Kutoka katika kilelel cha kilima kidogo mnaona magari makubwa ya mizigo na wanaume wengi wakiwa na misumeno. Tayari eneo kubwa la msitu limeshakatwa. Hamuwajui watu hawa ni kina nani? Nani aliyewaruhusu kukata msitu wenu? Kwa nini hakuna aliyewaeleza kuhusu jambo hili?

1. Je, tukio hili linafafanua unachokifikiria kuwa ni ridhaa inayotolewa "kabla"?
2. Je, ni hatua gani ambazo jamii hii inatakiwa kuchukua kuhusiana na tukio hili?
3. Kama jamii imekuwa katika hali hii kabla walifanya nini? Matokeo yake yalikuwa nini

# KIAMBATISHO E: MASWALI KWA AJILI YA ZOEZI LA 9

1. Je, serikali inashauriana na jamii?
2. Je, makampuni yanashauriana na jamii?
3. Je, serikali ina sheria ambazo zinailinda jamii?
4. Je, sheria zinaheshimiwa na makampuni?
5. Je, sheria zinaheshimiwa na serikali?
6. Je, jamii inapewa taarifa?
7. Je, jamii inapewa taarifa mapema?
8. Je, jamii inashirikishwa katika ufanyaji wa maamuzi?
9. Je, jamii ni wafanyaji wa maamuzi?
10. Je, jamii inafaidi?

# KIAMBATISHO F:
# MIFANO YA UTAFITI WA TATHMINI NA FIKRA BINAFSI

## UTAFITI WA TATHMINI YA MSHIRIKI

Wewe ni: mwanamke /mwanamume [zungushia wewe ni nani]

Wewe ni: Mtu mzima / kijana / mzee [zungushia wewe ni nani]

Trehe: ____________________

Jina la jamii yako: ____________________

| | | |
|---|---|---|
| Ninaelewa FPIC ni nini: | Hapana/ kidogo | ndiyo/sana |
| Ninaelewa jinsi FPIC inavyoweza kulinda haki na maslahi yangu: | Hapana/ kidogo | ndiyo/sana |
| Ninajisikia kwamba jamii yangu sasa ina uwezo wa kufanya maamuzi na kuchukua hatua kwa pamoja ili kulinda haki na maslahi yetu yote: | Hapana/ kidogo | ndiyo/sana |
| Niliweza kushiriki kikamilifu katika programu ya mafunzo: | Hapana/ kidogo | ndiyo/sana |
| Nilikuweza kushirikisha mawazo yangu wakati wa mafunzo: | Hapana/ kidogo | ndiyo/sana |
| Nilijisikia kwamba washiriki wengine walinisikiliza wakati nilipokuwa nazungumza na waliheshimu mawazo yangu: | Hapana/ kidogo | ndiyo/sana |

Je, ulifurahia nini zaidi kuhusiana na mafunzo?

____________________

____________________

____________________

Je, kuna kitu chochote ambacho hukukipenda au ambacho wafundishaji wangekifanya tofauti?

____________________

____________________

____________________

Hatua gani utazichukua kama matokeo ya kushiriki katika mafunzo haya?

____________________

____________________

____________________

## TATHMINI YA WAKUFUNZI YA KUJIPIMA BINAFSI

Tarehe ya mafunzo: ______________________________

Jina la jamii/mahali pa mafunzo: ______________________________

Jumla ya washiriki: ______________________________

Idadi ya wanawake: ______________ Idadi ya wanaume: ______________

1. Je, unadhani washiriki wameboresha uelewa wao kuhusu FPIC kutokanana kushiriki katika programu ya mafunzo? Kama sio, kwa nini unadhani imekuwa hivyo?

______________________________

______________________________

2. Nini kilifanyika vizuri?

______________________________

______________________________

3. Je, wanawake walishiriki vizuri? Toa baadhi ya mifano ya jinsi wanawake walivyoshiriki.

______________________________

______________________________

4. Je, kulikuwa na vikwazo vyovyote katika ushiriki wa wanawake? Je, vikwazo hivyo vinaweza kukabiliwa vipi wakati ujao?

______________________________

______________________________

5. Je, ulikuwa na uwezo wa kupata mkataba na jamii (Zoezi la 2) kuhusu namna washiriki wanavyopaswa kuenenda wakati wa programu ya mafunzo? Je, hii ilikusaidia kuhakikisha kila mmoja anashiriki kikamilifu?

______________________________

______________________________

6. Je, una uwezo wa kushughulikia mgogoro wowote au kutokukubaliana ambako kunaweza kutokea kati ya washiriki?

______________________________

______________________________

7. Je, ulikuwa na uwezo wa kujibu maswali yote ya washiriki waliyokuwa nayo kuhusu FPIC, haki za jamii au usimamizi wa rasilimali? Je, ni taarifa gani za nyongeza unazotaka programu ya mafunzo ya FPIC iziwasilishe wakati ujao?

______________________________

______________________________

8. Je, washiriki wamejenga hatua ambazo unadhani zitatekelezwa na zina madhara chanya kwa wanajamii wote?

______________________________

______________________________

9. Je, kuna jambo lolote unalodhani halikufanya kazi vizuri?

______________________________

______________________________

10. Ukifikiria hayo hapo juu, je, kuna kitu chochote unachodhani utakifanya vizuri au tofauti wakati ujao? Je, unahitaji rasilimali za nyongeza? Fikiria kuhusu vyote upangaji na uwasilishaji wa programu ya mafunzo; na programu ya mafunzo na mazoezi.

______________________________

______________________________